

**UCHANGANUZI MAKOSA NA MUUNDO SENTENSI: ULINGANISHO WA
SENTENSI SAHILI ZA KISWAHILI SANIFU NA ZA KISUBA**

NA

BEATRICE AKOTH KISAKWAH

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA
SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

2014

UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa kwa mahitaji ya shahada katika Chuo kikuu kingine chochote.

Sahihi -----

BEATRICE AKOTH KISAKWAH

TAREHE

(MTAHINIWA)

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu tukiwa wasimamizi wa kazi hii wa Chuo Kikuu Cha Nairobi.

Sahihi -----

PROF. OKOTH OKOMBO

TAREHE

(MSIMAMIZI)

Sahihi -----

DKT. JEFWA MWERI

TAREHE

(MSIMAMIZI)

TABARUKU

Tasnifu hii naitabarukia wanangu wpendwa Nicole, Neil na Malia pamoja na mume mpendwa Erastus Nyagwa. Namshukuru ghaya Erastus ambaye alinihimiza kila mara maisha yalipokuwa magumu kama mawe. Aidha alistahimili upweke na ukiwa ulioathiri hali ya kawaida katika harakati yote ya masomo yangu, kongole kipenzi cha roho yangu.

Vilevile, naitabarukia wazazi wpendwa marehemu Martine Kisakwah na Herine Kisakwah walionilea na kunifunza thamani ya mtoto wa kike kupata elimu.

Mama, Mola akupe maisha marefu.

SHUKRANI

Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo wa kutimiza ndoto yangu ya kupata shahada ya uzamili katika Kiswahili.

Nawashukuru wahadhiri wote wa Idara ya Isimu kwa kazi yao nzuri kupitia kwa nasaha yao.

Aidha nawashukuru Prof. Okoth Okombo, Dkt. Jefwa Mweri na Dkt. Iribe Mwangi walionipa ushauri na maelekezo ili nifanikishe kazi hii.

Pia nawashukuru marafiki zangu Maggy Karanja, Julius Kirubi, Furaha Mbetsa, Sr. Teresia (Sisto) kwa kunihimiza ili nisife moyo japo maisha yalikuwa yamechukua mkondo tofauti.

Kadhalika, nawashukuru ndugu na dada zangu David, Felix, Lucy na Ruth Kisakwah walionipa moyo wa kupiga hatua maishani.

Nawashukuru wote waliofanikisha utafiti huu. Asante sana na Mola awazidishie.

YALIYOMO

UNGAMO.....	ii
TABARUKU	iii
SHUKRANI.....	iv
UFAFANUZI WA MSAMIATI NA BAADHI YA SENTENSI.....	ix
IKISIRI	xiv
SURA YA KWANZA	1
UTANGULIZI	1
1.1 Usuli wa mada.....	1
1.3 Madhumuni ya utafiti	5
1.5 Umuhimu wa utafiti	6
1.7.4 Yaliyoandikwa kuhusu makosa	10
1.8.3 Mikakati ya kuwasiliana katika lugha ya pili	17
1.8.4 Ujumlishaji mno wa kiholela.....	17
1.9 Mbinu za Utafiti	19
1.9.1 Ukusanyaji data	19
1.9.2 Mahali pa utafiti.....	20
1.9.3 Mbinu ya utafiti	21
1.9.4 Uchanganuzi wa data.....	21
1.10 Hitimisho.....	22
SURA YA PILI.....	23
UCHANGANUZI LINGANUZI WA SENTENSI ZA KISUBA NA KISWAHILI	
SANIFU	23
2.0 Utangulizi	23
2.1 Viambajengo vinavyounda sentensi.....	24

2.1.1	Nomino za Kisuba	24
2.1.2	Jedwali linaloashiria Ngeli za Kisuba na za Kiswahili.....	27
2.1.3	Mifano ya viambishi vya nomino	30
2.1.4	Uainishaji wa nomino kisintaksia.....	31
2.1.5	Jedwali la vipatanishi vya Kisuba na Kiswahili sanifu	32
2.1.6	Vipatanisho vya Kiswahili sanifu na za Kisuba	34
2.2	Vivumishi	35
2.2.1	Vivumishi vya -a unganifu	35
2.2.2	Muundo wa viunganifu (-a) ni kama ifuatayo	35
2.2.3	Matumizi ya kiunganifu (-a) katika sentensi za Kisuba na Kiswahili sanifu ...	36
2.2.4	Vivumishi vionyeshi.....	37
2.2.5	Vivumishi vionyeshi katika ngeli za Kisuba na za Kiswahili sanifu	38
2.2.6	Mifano ya matumizi ya vivumishi vionyeshi katika sentensi.....	39
2.2.8	Vivumishi vya sifa.....	40
2.2.9	Vivumishi vya idadi visivyodhahiri	42
2.3	Viwakilishi	44
2.3.1	Viwakilishi vya nafsi	44
2.3.2	Jedwali la viwakilishi nafsi.....	44
2.4	Vitenzi	45
2.4.1	Sentensi zinazosheheni viarifu vya Kisuba na Kiswahili sanifu	47
2.4.2	Vikanushi vya vitenzi vya Kisuba na Kiswahili.....	48
2.4.3	Mifano ya sentensi zinazosheheni viambishi	49
2.4.4	Sentensi za Kisuba na Kiswahili sanifu zinazosheheni upatanisho wa kisarufi	50
2.4.5	Viambajengo vya sentensi	50
2.4.6	Uchanganuzi wa viambajengo.....	51

2.5.1 Kiima	53
2.5.2 Kiarifa.....	54
2.6 Uchanganuzi kikategoria.....	55
2.6.1 Elementi za Kirai Nomino.....	58
2.6.2 Sifa za kundi Tenzi katika Kisuba na Kiswahili sanifu.....	58
2.7 Hitimisho.....	59
SURA YA TATU	61
UCHANGANUZI WA MAKOSA.....	61
3.0 Utangulizi	61
3.1 Makosa ya Kifonolojia	61
3.1.1 Udondoshaji au uchopekaji wa sauti	62
3.2 Makosa ya kimofolojia.....	64
3.3 Makosa ya kisintaksia	64
3.4 Makosa ya kisemantiki.....	64
3.5 Uchanganuzi wa makosa ya kisintaksia	65
3.5.1 Makosa yanayohusu matumizi mabaya ya vivumishi vionyeshi.....	66
3.5.2 Vivumishi vya sifa.....	67
3.5.3 Vivumishi viunganifu.....	68
3.5.4 Vivumishi vya pekee ‘o – te’	69
3.5.5 Uhamisho wa msamiati	70
3.5.6 Upatanisho wa Kisarufi	71
3.6 Hitimisho.....	72
SURA YA NNE.....	73
UCHANGANUZI WA DATA	73
4.0 Utangulizi	73

4.1 Idadi ya makosa ya kisintaksia ikilinganishwa na makosa yasiyo ya kisintaksia...	73
4.2 Idadi ya makosa ya kisintaksia yanayosababishwa na athari ya lugha ya kwanza	75
4.3 Hitimisho.....	77
SURA YA TANO.....	78
MATOKEO NA MAPENDEKEZO.....	78
5.0 Utangulizi.....	78
5.1 Muhtasari wa matokeo	78
5.2 Mapendekezo	80
5.3 Hitimisho.....	80
MAREJELEO	81
KIAMBATISHO.....	85

UFAFANUZI WA MSAMIATI NA BAADHI YA SENTENSI

Nomino za kisuba

Katonda - Mungu

Omulozi - mchawi

Omugerezi - mwalimu

Omwana - mtoto

Omwaala - msichana

Nomino za wanyama

Efarasi – farasi

Ekikerewe - chura

Embuzi - mbuzi

Emvya – samaki

En'gombe - n'gombe

Nomino ya kawaida

Igi – mayai

Isaka - kichaka

Itoke - ndizi

Ekitabu - kitabu

Esaafu - matunda

Emvwiri - nywele

Entewe - kiti

Muchiro - sokoni

Musukuli - shuleni

Okuria – chakula

Omioyo - moyo

Omusiri - shamba

Omuti - mti

Uwusara - uji

Vitenzi vya Kisuba

Aeere - alimpa

Afumre - amepika

Amenyere – anaishi

Aingire - ameingia

Anywa - anakunywa

Ariire - amekula

Eria – anakula

Fumba - pika

Galuka - ruka

Gwiire - anguka

Jojia - andika

Nyemba - imba

Nyozia - fua

Seka - cheka

Wanoga - kuchuma

Viwakishi nafsi

Mimi - inze

Nyinyi – inywe

Sisi - ifue

Wewe – iwue

Yeye – iyie

Vivumishi

Omukalu - mkubwa

Omulootu - mzuri

Ukalu - Sana

Uwiwi - vibaya

Wuwisi - mbichi

Majina ya watu

Adawo

Asadhi

Asweto

Kicha

Kungu

Mokami

Nyakiamo

Ogwada

Syongo

Vivumishi vionyeshi

Guno - huu

Kino - hiki

Ono – Huyu

Riria - hilo

Vivumishi vimilikishi

Kiange – changu

Wange - wangu

Wiange - vyangu

Sentensi za Kisuba na Kiswahili

Amiino giifu no amalootu – Meno yetu ni mazuri

Amiino goona gaonike - meno yote yameharibika

Awagaka wanywa uwusara - wazee wanakunywa uji

Awaala wagonzizie okuiwaka amavuta - wasichana wanapenda kujipaka mafuta

Awaana wanoga esaafu ku omuti - watoto wanachuma matunda mitini

Awatu woona waazire - watu wote wamekuja

Ekikerewe kidumakiduma - chura anarukaruka

Emiti giona gizakukengwa - miti yote itakatwa

Eno ne entewe eya omugerezi - hiki ni kiti cha mwalimu

Entewe zino zionike uwiwi - viti hivi vimeharibika vibaya

Emvwiri ziona zisukrwe geza - nywele zote zilisukwa vizuri

Entikiri eno agingra amazi - Punda huyu amebeba maji

Ewifunguo ewia enyumba iifu witekre - vifunguo vya nyumba yetu vimepotea

Ewikapu wino no ewia gukwa - vikapu hivi ni vya nyanya

Ewirato woona wilootu wionike - viatu vyote vizuri vimeharibika

Igondi rino ritekre kumwai - kondoo huyu amempotelea mchungaji

Irino riange ne ilootu ikalu - jino langu ni zuri sana

Katonda amenyere kuegulu - Mungu anaishi mbinguni

Omwana omulootu agwiire aasi - mtoto mzuri ameanguka chini

Omwana ono ariire owita wuona - mtoto huyu amekula ugali wote

Omwana wange omulooti agwiire uwiwi ukalu - mtoto wangu mzuri ameanguka vibaya
sana

Ono no omwana wa senge - huyu ni mtoto wa shangazi

Wino ni ewikapu wiange - hivi ni vikapu vyangu

IKISIRI

Wanafunzi wanaojifunza lugha ya pili hufanya makosa mengi yakiwemo matamshi mabaya ya maneno. Kutokana na hali hiyo, wanaisimu wamekuwa katika mstari wa mbele kubaini chanzo cha makosa na vilevile kubuni mbinu faafu zinazochangia katika kutatua matatizo hayo.

Utafiti huu ulinuia kutimiza malengo yafuatayo mathaalan; kuainisha makosa ya kisintakisia katika kazi za wanafunzi kutoka kisiwani Mfangano, kuhakiki makosa yanayojitokeza katika tungo za wanafunzi na pia kubaini kiwango cha makosa yanayosababishwa na athari ya lugha ya kwanza. Kwa hivyo, kutokana na matokeo yetu, tulibaini kuwa makosa mengi hujitokeza katika tungo za wanafunzi na pia ni wazi kuwa makosa hujidhihirisha katika vipashio vyote vya lugha, ijapokuwa kwa asilimia tofauti

Nadharia iliyotumiwa katika kazi hii ni nadharia ya uchanganuzi linganuzi ambayo huangazia ulinganuzi wa mifumo ya lugha mbili ili kubaini tofauti zinazojitokeza kati ya lugha hizo. Kadhalika nadharia hii huchukulia kuwa makosa katika lugha ya pili husababishwa na athari ya lugha ya kwanza.

Kwa muhtasari, kazi hii imemulika makosa ya kisintakisia ya wanafunzi kutoka kisiwani Mfangano na aidha kubuni namna ya kukabiliana na makosa yanayosababishwa na lugha ya kwanza.

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.1 Usuli wa mada

Kwa mujibu wa Kapinga (1983) sentensi ni kipashio kikubwa kuliko vipashio vya kiisimu na huwa na wazo kamili. Sentensi ni sehemu ya sarufi ambayo aghalabu hujisimamia kimaana. Mara nyingi, sentensi huwa na maana ambayo huweza kuwa ni taarifa, ombi, masharti au hata amri. Kwa hivyo sentensi ni kipashio muhimu kwa kuwa husababisha kuwepo kwa mawasiliano, ambayo ni kiungo muhimu katika maisha ya binadamu kwa jumla.

Waandishi wengi wamefafanua sentensi kwa njia anuwai. Mathaalan, Richard et al (1985) anasema sentensi ni dhana asili ya lugha ambayo hufafanuliwa kudhihirisha sehemu ya sarufi yenye neno moja au zaidi inayosimamia wazo kamili. Kwa mujibu wa Radford (1997) sentensi ni sehemu ya sarufi ambayo hujisimamia kisintaksia na huwa na kiima na kiarifa ambacho kina kitenzi kimoja au zaidi. Kutokana na ufafanuzi wa waandishi hawa, ni dhahiri shahiri kuwa, sentensi ni sehemu ya sarufi, yenye kiima na kiarifa na vilevile husimamia wazo kamili. Kadhalika sentensi hudhihirisha sehemu ya leksia yenye neno moja au hata zaidi. Fauka ya hayo, sentensi huweza kufafanuliwa kwa kuzingatia muundo wake ambao huwa ni aina tofauti za sentensi. Aidha, sentensi pia hufafanuliwa kwa mujibu wa dhima yake kwa mfano, sentensi zinazodhihirisha ombi, swali, amri, mshangao na taarifa. Kwa hivyo, ufafanuzi huu wote umejikita kwenye miundo na uamilifu wa sentensi, hata hivyo utafiti huu umepiga hatua kwa kuangazia kwa jumla kategoria mbalimbali za maneno katika sentensi.

Massamba (2004), Obuchi na Mukhwana (2010) na Gary Forlini et al (1990) wameainisha aina nyingi za sentensi. Kulingana na wataalam hawa, sentensi sahili husheheni kundi nomino na kundi tenzi. Kazi ya waandishi hawa haswa kuhusu miundo ya sentensi imekuwa muhimu katika utafiti huu kwa kuwa muundo wa sentensi umeangaziwa na kutiliwa mkazo kwa kina katika kazi hii.

Maadam kazi hii imehakiki ulinganisho wa sentensi za lugha ya Kiswahili sanifu na Kisuba, ni muhali kuelezea usuli wa Kisuba kwa muhtasari. Abasuba ni Wabantu waliogura nchini Uganda kama wakimbizi kati ya miaka 1780-1820. Waligura Uganda na kuja nchini Kenya. Waliishi kwenye visiwa vya Rusinga, Mfangano, Kaksingri, Gwasi na pia maeneo ya Muhuru na Suna. Lugha ya Kisuba ina lahaja tatu. Lahaja hizo nazo ni pamoja na: Kisuba inayozungumzwa na wakazi wa Muhuru na Suna Mashariki. Wakazi wa Kaksingri ambao huitwa *Abakune* huzungumza lahaja ya *Orukune* ilhali wakazi wa Mfangano ambao wajaluo huwaita '*Olumwa*' hutumia lahaja ya Olusuba. '*Olumwa*' imetokana na neno la Kijaluo '*Jamwa*' lenye maana asiye mwenyeji. Utafiti huu umetumia lahaja ya Olusuba. Lahaja hii haswa itaitwa Kisuba madhali ndio mfumo wa Kiswahili unaotumiwa kuashiria lugha mbalimbali za ulimwengu. Aidha, lahaja ya Mfangano ambayo ni Olusuba haitumii kiambishi 'ki' inapoashiria lugha mbalimbali za ulimwengu.

Licha ya hayo, utafiti huu umetumia nadharia ya uchanganuzi linganuzi ambayo imo ndani ya nadharia pana ya uchanganuzi makosa. Nadharia hii imetusaidia kuainisha makosa yaliyo kwenye kazi za wanafunzi. Aidha, *Dictionary of language teaching and applied linguistics* (2000) pia imeainisha makosa ya wanafunzi kwa njia ifuatayo: yale makosa ya kifonolojia yanayohusu matamshi, makosa ya kileksika ambayo huhusu

msamiati na vilevile kuna makosa ya kisarufi ambayo hujumuisha mpangilio wa maneno katika tungo. Kadhalika makosa mengine hutokana na tafsiri ambapo maana ya msemaji au lengo la msemaji hukosa kueleweka na msikilizaji. Hatimaye, kuna makosa yanayohusu kitengo cha pragmatiki ambayo huchunguza maana kulingana na miktadha ya matumizi ya neno.

Kwa kuwa uchanganuzi makosa hujumuisha eneo pana la utafiti, kazi hii imejikita kwenye kipengele cha uchanganuzi linganuzi. Nadharia ya uchanganuzi linganuzi imo ndani ya nadharia pana ya uchanganuzi makosa. Nadharia hii huchunguza makosa yanayosababishwa na tofauti zinazojitokeza baina ya lugha mbili kwa mfano Kisuba na Kiswahili. Kadhalika kazi hii imelinganisha sentensi za Kisuba na Kiswahili. Ulinganisho wa lugha mbili umewezesha kubaini sifa zinazozitambulisha na kuzitofautisha lugha hizo.

Kutokana na maelezo ya hapo juu, tunabaini kuwa utafiti huu umechunguza uhusiano uliopo kati ya lugha hizi mbili kwa kuwa tafiti za awali zinabaini kuwa Kiswahili na Kisuba zina sifa zinazozifananisha. Pamoja na hayo, Guthrie (1971) anasema kuwa, Kiswahili ni lugha ya Kibantu na hivyo basi kinastahili kuainishwa katika kopo moja na lugha za Kibantu. Aidha kwa mujibu wa Guthrie, sifa zinazopatikana katika lugha za Kibantu ni kuwa nomino zake hupangwa kwenye makundi yanayoitwa ngeli. Aidha sentensi zao huonyesha upatanifu wa kisarufi. Pamoja na hayo, lugha za Bantu pia zimebainika kuwa zina viambishi vinavyoashiria hali tofauti. Viambishi hivyo huwekwa kwenye vivumishi na vitenzi ili kudhihirisha upatanifu wa kisarufi. Hata hivyo, ijapokuwa lugha za Kisuba na Kiswahili zina mwingiliano wa kiasi fulani, kuna viambajengo ambavyo ni tofauti katika kiwango cha sentensi. Kwa mfano katika lugha ya

Kiswahili, kuna aina ya vivumishi ambavyo hupatikana katika lugha hiyo ilhali vivumishi hivyo kukosekana katika lugha ya Kisuba. Vivumishi hivyo ni vile vinavyoashiria vitu visivyokuwa karibu na mzungumzaji wala msemaji.

Guthrie ameongezea kuwa, Kiswahili na Kisuba ni lugha za Kibantu kwa hivyo zinastahili kusheheni sifa zinazofanana. Mbali na hayo, nomino zao pia zinastahili kupangwa kwenye makundi yanayoitwa ngeli. Fauka ya hayo yote, japo lugha hizi mbili zina sifa zinazoshabihiana, makosa mengi bado yanashuhudiwa katika tungo za wanafunzi. Kwa sababu hiyo, kazi hii imetathmini tofauti zinazojitokeza katika kiwango cha sarufi ili kubaini chanzo cha makosa na kadhalika kutathmini jinsi ya kukabiliana na makosa katika tungo za wanafunzi.

1.2 Swala la utafiti

Wanafunzi katika shule ya Nyahera kisiwani Mfangano wanafanya makosa mengi katika uandishi wa tungo. Vilevile tukitazama matokeo ya mtihani, inabainika kuwa wanafunzi katika shule hii wanakumbwa na matatizo wanapoandika insha. Aidha, imebainika kuwa makosa huwa na visababishi vingi mbali na athari ya lugha ya kwanza Corder (1971). Kadhalika ameongezea kuwa lugha wakati mwingine huweza kuwa na utaratibu usiofuata mfumo wa kawaida ambayo husababisha makosa katika lugha husika. Richard (1971) aidha amezungumzia swala la makosa na kusema kuwa makosa mengi katika tungo za wanafunzi husababishwa na uhamisho. Otiende (2013) naye amechunguza mifanyiko ya kifonolojia kati ya Kisuba na Kiswahili sanifu. Kwa hivyo, japo wataalam wengi wameangazia swala hili la makosa, kufikia sasa hakuna thibitisho kuwa utafiti kuhusu

makosa ya kisintaksia yameshughulikiwa na hilo ndilo pengo ambalo utafiti huu umeweza kuziba. Kwa sababu hiyo, utafiti huu umeweza kujibu maswali yafuatayo:

- Je, makosa yapi ya kisintaksia ambayo wanafunzi hufanya katika uandishi wa tungo?
- Je, ni makosa yapi husababishwa na tofauti za kisintaksia baina ya Kiswahili sanifu na Kisuba?
- Ni kiwango kipi cha makosa ambacho husababishwa na lugha ya kwanza.

1.3 Madhumuni ya utafiti

1. Kuainisha makosa ya kisintaksia katika kazi za wanafunzi kutoka kisiwani Mfangano, shule ya Nyahera.
2. Kuhakiki makosa yanayojitokeza katika tungo za wanafunzi.
3. Kubaini kiwango cha makosa yanayosababishwa na lugha ya kwanza.

1.4 Haipotesia

1. Kazi za wanafunzi kisiwani Mfangano, shule ya Nyahera hudhihirisha makosa ya kisintaksia.
2. Tofauti za kisintaksia kati ya Kiswahili sanifu na Kisuba huathiri matumizi ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi kisiwani Mfangano, shule ya msingi ya Nyahera.
3. Takriban asilimia arubaini ya makosa ya kisintaksia husababishwa na athari ya lugha ya kwanza.

1.5 Umuhimu wa utafiti

Kutokana na uchunguzi wa awali, hakuna thibitisho kuwa tafiti zozote zimewahi kufanywa kuhusu ulinganisho wa sentensi sahili za Kiswahili sanifu na Kisuba ili kubaini athari ya Kisuba katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Aidha kazi hii imebaini chanzo cha makosa katika tungo za wanafunzi kutoka kisiwani. Mfanganano pia kuorodhesha namna ya kukabiliana na makosa hayo. Kadhalika, ni dhahiri kuwa alama wanazozipata wanafunzi katika somo hili la Kiswahili ni za chini na pia tungo zao zinasheheni makosa chungu nzima. Kutokana na sababu hizo, kazi hii ina manufaa kwa kuwa imechunguza chanzo cha makosa na vilevile kubaini jinsi ya kukabiliana na makosa hayo.

1.6 Upeo wa utafiti

Utafiti huu umechunguza makosa yanayojitokeza katika tungo za wanafunzi. Makosa hayo haswa ni yale yanayosababishwa na tofauti zilizopo baina ya Kisuba na Kiswahili sanifu. Kadhalika shule moja ndiyo imehusishwa katika utafiti huu kwa kuwa muda tulionao hautoshi kushughulikia zaidi ya shule moja. Shule hiyo ni shule ya msingi ya Nyahera. Shule hiyo imependekezwa kwa sababu wanafunzi wake wana uwezo wa kuzungumza Kisuba bila tatizo lolote na kadhalika wanafunzi hao hutumia lugha hiyo wanapokuwa nyumbani. Kwa hivyo kutokana na hali hiyo, tunachukulia kuwa lugha yao ya kwanza haijaathirika sana na lugha nyingine. Aidha, darasa la saba ndilo limehusishwa katika utafiti huu kwa kuwa wanafunzi wa darasa la nane wanajiandaa kufanya mtihani wao wa kitaifa ilhali wanafunzi wa darasa la kwanza hadi darasa la sita hawana umilisi katika lugha ya Kiswahili ikilinganishwa na wanafunzi wa darasa la saba. Pamoja na hayo, sio kila mwanafunzi amehusishwa katika uandishi wa insha bali wale ambao

hususan hutumia Kisuba pekee wanapokuwa nyumbani. Data hiyo tumeipata kupitia kwa kuwahoji kila mwanafunzi kutoka darasa hilo.

Aidha kazi hii imelinganisha sentensi sahili za lugha mbili yaani Kisuba na Kiswahili sanifu kwa kuwa kipengele hiki cha sintaksia hakijawahi kushughulikiwa na mtafiti yeyote. Pamoja na hayo, nadharia iliyotumiwa katika uainishaji wa makosa ilikuwa uchanganuzi linganuzi ambayo imo ndani ya nadharia pana ya uchanganuzi makosa. Nadharia ya uchanganuzi makosa ni pana mno, na huenda tungekosa kutimiza malengo yetu ya utafiti ikiwa tungeitumia. Vilevile, sio makosa yote yaliyopatikana katika tungo za wanafunzi yalishughulikiwa bali yale ya kisintaksia na vilevile yale yanayosababishwa na athari ya lugha ya kwanza pekee. Pamoja na hayo, nadharia ya sarufi mapokeo na sarufi miundo pia ilitufaidi mno katika uchanganuzi wa sentensi. Kwa hivyo kupitia kwa nadharia ya sarufi miundo, tuliweza kugawanya sentensi kwa kutumia dhana ya upanuzi uliotuwezesha kuchunguza sentensi za Kisuba na za Kiswahili sanifu kwa kina. Aidha nadharia ya sarufi mapokeo ilituwezesha kuainisha viambajengo kadhaa vinavyounda sentensi.

Fauka ya hayo, ijapokuwa kipengele cha sintaksia kimeangaziwa mno katika utafiti huu, mofolojia pia imetufaa katika kazi hii kwa kuwa kuna baadhi ya maswala yanayohusu uundaji wa maneno na matumizi ya viambishi ambavyo haviwezi kushughulikiwa kwa kutumia kipengele cha sintaksia.

Licha ya hayo, sio watu wote kutoka Mfangano walihojiwa kuhusu lugha ya Kisuba bali tuliwahoji watu kadhaa na hatimaye tukamteua mtu mmoja pekee. Mtu huyo aliteuliwa kwa sababu yeye pekee kati ya watu wengi ndiye aliyekuwa na uwezo wa kuzungumza

lugha hizo mbili (Kiswahili na Kisuba) kwa ufasaha na kadhalika mtu huyo alikuwa na uwezo wa kuandika pia.

1.7 Yaliyoandikwa kuhusiana na mada

Tumepitia kazi mbalimbali zinazorejelea mada hii. Dhana ya sentensi imefafanuliwa kwa njia anuwai. Kadhalika, tumeangazia yaliyoandikwa kuhusu mwingiliano baina ya lugha mbili na pia athari ya lugha ya kwanza katika lugha ya pili.

1.7.1 Yaliyoandikwa kuhusu mwingiliano baina ya lugha mbili

Curtain (1990) anasema, wanafunzi wanaojifunza lugha ya pili ni vyema waelewe miundo msingi ya lugha hiyo na vilevile matamshi bora.

Kwa mujibu wa Cook (1969, 1971) na Ervin-Trip (1974) uhusiano uliopo kati ya lugha mbili ni muhimu kwa kuwa lugha huathiriana. Aidha wameongezea kuwa, lugha ya kwanza huathiri ujifunzaji wa lugha ya pili.

Kazi ya waandishi hawa ilitufaa katika utafiti huu kwa kuwa kazi yao ilitilia mkazo swala la mwingiliano baina ya lugha mbili na pia kuangazia athari ya lugha ya kwanza katika lugha ya pili. Kwa hivyo, kazi yao imetuwzesha kulinganisha na kulinganua sentensi kadhaa za Kisuba na za Kiswahili sanifu. Ulinganisho huo umefanikisha kubaini kiwango cha athari kati ya lugha hizo mbili. Aidha ulinganisho huo haujatusha umbo la sentensi pekee bali pia viambajengo vya sentensi. Kwa hivyo, ulinganisho wa sentensi za lugha hizo umechangia pakubwa katika kubaini chanzo cha makosa katika tungo za wanafunzi. Vilevile, kazi yao pia ilikuwa data toshelezi ya kudondoa maneno yenye athari za lugha

ya kwanza na kisha kuzilinganisha ili kupata tofauti zinazojitokeza kati ya lugha hizo mbili.

1.7.2 Yaliyoandikwa kuhusu athari ya lugha ya kwanza katika lugha ya pili

Otiende (2013) ameshughulikia swala la athari ya lugha ya kwanza katika lugha ya pili. Aidha aliangazia mifanyiko ya kifonolojia kati ya Kisuba na Kiswahili sanifu. Kupitia kwa kazi yake, imebainika kuwa kuna tofauti za kimofolojia kati ya lugha hizo mbili ambazo huathiri matumizi ya lugha ya Kiswahili miongoni mwa wazungumzaji wa Kisuba. Pia amethibitisha kuwa kuna baadhi ya fonimu ambazo hutofautiana katika lugha hizo mbili na hivyo kusababisha athari fulani katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Kazi ya mtafiti huyu imetufaa pakubwa ijapokuwa haijashughulikia kipengele cha sintaksia ambacho ni kitovu cha kazi hii. Sintaksia huangazia sentensi kwa kina na sheria za uundaji wa sentensi. Pamoja na hayo, kipengele hicho huchunguza viambajengo anuwai vinavyounda sentensi na jinsi viambajengo hivyo huathiriwa katika sentensi.

1.7.3 Yaliyoandikwa kuhusu dhana ya sentensi

Kwa mujibu wa Mutua na Mungwoki (2010) sentensi ni tungo iliyo na miundo ya kiima na kiarifa na yenye kutoa maana kamili. Waandishi hawa wamefafanua sentensi kwa mujibu wa muundo wake na kwa kurejelea sentensi kama kundi la maneno. Kulingana na waandishi hawa, sentensi sahili ni sentensi zenye kishazi kimoja na huwakilisha wazo moja tu. Kadhalika, Gary Forlin et al (1990) na Habwe na Karanja (2004) wanasema, sentensi sahili ni sentensi ambayo ina kitenzi kikuu kimoja au kishazi kikuu kimoja. Obuchi na Mukhwana (2010) kwa upande mwingine wamefafanua sentensi na kutilia

mkazo kwenye sifa zao. Wanasema, sentensi husheheni kishazi huru kimoja ambapo kishazi huru hicho ndicho huunda kundi nomino pamoja na kundi tenzi.

Kwa mujibu wa Massamba na wenzake (1999) na Deen (2002) lugha za Bantu hushabihiana kimuundo na kisifa. Aidha wanasema kuwa, lugha hizo huwa na mfuatano wa viambishi na mizizi. Viambishi hivyo huweza kutokea awali au baada ya mizizi.

Kazi ya waandishi hawa imekuwa na mashiko makubwa katika utafiti wetu kwa sababu viambajengo vya sentensi vilivyotajwa na wataalam hawa ndivyo vimekuwa nguzo za utafiti huu kwa jumla. Mbali na hayo, dhana ya sentensi waliyoshughulikia ndiyo imetufaa mno katika kazi hii kwa kuwa imetuwezesha kubaini viambajengo vya sentensi na pia utambuzi wa tofauti zinazojitokeza kati ya Kisuba na Kiswahili sanifu. Kadhalika, kazi yao imerahisisha utafiti huu kwa kuwa walifafanua muundo wa sentensi kwa jumla na pia kuangazia viambishi vinavyopachikwa kwenye mizizi.

1.7.4 Yaliyoandikwa kuhusu makosa

Kwa mujibu wa Swan na Smith (1987) makosa husababishwa na mwingiliano kati ya lugha mbili. Mwingiliano huo ndio husababisha utata na kutatiza matumizi ya lugha.

Norrish (1983) na Brown (1987) kwa upande mwingine wanachukulia kuwa makosa yanayofanywa na wanafunzi yanafaa kutazamwa kama jambo la kawaida. Kadhalika wanasema kuwa, makosa yanaashiria hali ya ukuaji na maendeleo katika shughuli nzima ya ujifunzaji wa lugha fulani. Aidha wameongezea kuwa, wanafunzi hufaidika wanapofanya makosa kwa kuwa wao hukosolewa na kupewa maelekezo faafu.

Kwa mujibu wa Corder (1967), makosa yana manufaa mengi kwa mfano, mwalimu hupata fursa ya kutathmini ikiwa mbinu anazozitumia ni faafu au la. Mbali na hayo,

mwalimu anapata kufahamu yale yote ambayo mwanafunzi wake amepata kujifunza ikiwemo vipengele ambavyo mwanafunzi wake hatambui katika lugha ya pili. Kadhalika mwalimu huwa na fursa ya kutathmini ikiwa malengo yake ya ufunzaji wa lugha yanafikiwa au la. Hatimaye, yeye hupata kubaini vipengele vinavyopaswa kutiliwa mkazo katika shughuli nzima ya ufunzaji wa lugha ya Kiswahili. Licha ya hayo, mwandishi huyu ametaja faida za makosa hayo kwa mtafiti mwenyewe. Anasema, mtafiti hupata kuelewa chanzo cha makosa na namna anuwai ya kukabiliana na makosa. Fauka ya hayo, mtafiti hupata kutambua aina tofauti za makosa na visababishi vyao. Kadhalika, mtaalam huyu ameeongezea kuwa, makosa hayahepukiki katika kazi za wanafunzi hivyo basi, mwanafunzi anafaa kupewa mwelekeo thabiti unaomuwezesha katika ujifunzaji wa lugha ya pili. Pia, anasema kuwa uchanganuzi makosa licha ya kuchunguza makosa ya wanafunzi, huangazia lugha husika kwa undani haswa kwa kumulika vipengele vingi vya lugha hiyo.

Richard (1971), Carroll (1971) na Swan na Smith (1987) vilevile wameshughulikia swala hili la makosa. Wanasema, makosa mengi hutokana na uhamisho. Kutokana na sababu walizozitoa, vipengele vya kiisimu huweza kuhamishwa kutoka lugha ya kwanza hadi lugha ya pili na hivyo kusababisha makosa katika lugha ya pili.

Mtazamo wa Selinker (1960) aidha umeshabihiana na wa wenzake, anasema, vipengele vya isimu vinavyohamishwa kutoka lugha ya kwanza hadi lugha ya pili huathiri mfumo wa lugha ya pili.

Norrish (1983) na Brown (1987) japo hoja yao inashabihiana na ya Selinker, wamepiga hatua na kuongezea kuwa makosa yanafaa kuchukuliwa kama ishara ya maendeleo mwanafunzi anapokuwa katika harakati ya kujifunza lugha ya pili.

Aidha kwa mujibu wa Brown (2000), Corder (1973) na Larsen (1992) makosa huweza kujitokeza katika viwango vyote vya Isimu.

Waandishi wa FPESP (2004) pia wameshughulikia swala hili la makosa na mawazo yao kujumuishwa kwa njia ifuatayo. Makosa mengi katika lugha husababishwa na swala la uhamisho. Uhamisho ni utaratibu wa kisintaksia wa kukitoka katika lugha fulani kiambajengo cha tungo na kukitumia katika lugha nyingine. Kadhalika wameongezea kuwa, sio makosa yote husababishwa na athari ya lugha ya kwanza bali mengine husababishwa na visababishi vingi vikiwemo, mfumo wa lugha usiofuata utaratibu ya kawaida.

Mchango wa waandishi hawa ni muhimu katika utafiti huu kwa kuwa, vipengele hivyo vinavyohamishwa kutoka lugha moja hadi nyingine ndivyo vimeainishwa ili kupata kujua aina ya kosa na chanzo cha makosa kwa jumla. Kadhalika, wataalam hawa wamependekeza juhudi katika kuchunguza kila kosa pasipo kupuuza makosa mengine. Wazo hilo aidha ni muhimu katika kazi hii kwa kuwa kila kosa linastahili kuainishwa na vilevile kushughulikiwa ipasavyo.

1.7.5 Yaliyoandikwa kuhusu ufundishaji mbaya wa lugha ya pili

Selinker (1972) anawalaumu walimuwanaofundisha somo la Kiswahili. Anasema kuwa, wengi wao hawana umilisi wa lugha ya Kiswahili na pia baadhi yao hutumia mbinu zisizofaa wanapofunza lugha ya Kiswahili.

Kwa mujibu wa Krashen (1987) kielelezo mwafaka cha ufunzaji wa lugha kinahitajika. Aidha ameongezea kwamba, mwalimu anafaa kuwa kielelezo bora katika matumizi ya

lugha ya Kiswahili. Zaidi ya hayo, walimu wanahimizwa kupiga msasa lugha yao maadam makosa wanayoyafanya huigwa na wanafunzi wao.

Curtain (1990) aidha amesisitiza swala la matamshi. Anasema, mwalimu hafai kuathirika na lugha yake ya kwanza anapotamka maneno katika lugha ya pili.

Kazi za waandishi hawa ni muhimu kwetu kwa kuwa wametaja dhima ya mwalimu katika shughuli nzima ya ufunzaji wa lugha. Aidha, wamependekeza kuwa matatizo ya walimu yasipuuzwa na vilevile wawe kielelezo bora. Kwa hivyo, kielelezo bora kinachosisitizwa na wataalam hawa ndicho kimesisitizwa katika kazi hii kwani matamshi na matumizi mwafaka wa vipengele vya sentensi ndizo nguzo kuu katika kazi hii.

1.8 Misingi ya Nadharia

Waasisi wa nadharia ya uchanganuzi makosa ni Corder na wenzake (1960). Kwa mujibu wa nadharia hii, makosa husababishwa na visababishi vingi mbali na athari ya lugha ya kwanza. Aidha, nadharia hii inachangia katika kubaini mikakati ambayo hutumiwa na wanafunzi katika harakati za ujifunzaji wa lugha ya pili na vilevile, kutambua visababishi vya makosa na hata chanzo cha makosa mengi katika kazi za wanafunzi. Kwa mujibu wa Larsen (1992) nadharia ya uchanganuzi makosa huchunguza idadi ya makosa ya wanafunzi wanapojifunza lugha ya pili. Makosa hayo huwa sio yale yanayosababishwa na athari ya lugha ya kwanza pekee bali pia yale makosa ya kijumla.

Kulingana na Larsen (Ibid), makosa huweza kuwekwa katika vitengo kadhaa vikiwemo;

1. Ujumlishaji wa kiholela
2. Matumizi ya sheria zisizotoshelezi
3. Kutozingatia kanuni za lugha husika

4. Ubunifu wa fikra zisizo za kweli

Kwa kuwa nadharia ya uchanganuzi makosa ni pana mno, huenda tungekosa kutimiza malengo yetu ya utafiti ikiwa tungeitumia kwa hivyo, utafiti huu umetumia nadharia ya uchanganuzi linganuzi ambayo imo ndani ya nadharia pana ya uchanganuzi makosa. Uchanganuzi linganuzi huchunguza athari ya lugha ya kwanza kwenye lugha ya pili. Aidha nadharia hii huangazia ulinganuzi wa mfumo wa lugha mbili ili kubaini tofauti zinazojitokeza kati ya lugha hizo mbili. Pamoja na hayo, nadharia hii hususan huchukulia kuwa makosa katika lugha ya pili husababishwa na athari ya lugha ya kwanza. Vilevile, wanadharia hii wanasema kuwa nadharia hii ina uwezo wa kutambua chanzo cha kosa na pia kutabiri kutokea kwa makosa katika lugha ya pili.

Kwa jumla, nadharia ya uchanganuzi linganuzi husisitiza kwamba, makosa katika lugha ya pili husababishwa na uhamisho. Uhamisho hushuhudiwa kwa namna mbili. Mathaalan, uhamisho chanya na uhamisho hasi. Uhamisho chanya ni utaratibu wa kisintaksia wa kukitoa katika sehemu fulani kiambajengo cha lugha ya kwanza na kukitumia katika lugha ya pili. Uhamisho huo mara nyingi husababishi makosa yoyote katika lugha ya pili. Kadhalika, uhamisho hasi ni utaratibu wa kisintaksia wa kukitoa katika sehemu fulani kiambajengo cha lugha fulani na kukitumia katika lugha nyingine. Uhamisho huo ndio hususan husababisha makosa katika lugha ya pili.

Elis (1997) kwa upande mwingine ameshughulikia istilahi mbili ambazo ni uti wa mgongo wa kazi hii. Istilahi hizo ni, makosa na matatizo. Istilahi hizo aghalabu hutumika kwa njia ya kubadilishana ndiposa wanaisimu hawa wanazieleza kwa namna ifuatazo.

Kwa mujibu wa Brown (1987, 1993) na Corder (1967) kuna tofauti kati ya matatizo (error) na makosa. Mtazamo wao ni kuwa, makosa hutokana na matumizi mabaya ya

lugha na aidha hayana ruwaza na vilevile huweza kutokea katika hali yoyote. Kulingana na waandishi hawa, makosa hayana uzito wowote katika harakati ya ujifunzaji wa lugha ya pili. Aidha, wameongezea kuwa, makosa husababishwa na kutokuwa na umilisi wa kutosha katika lugha fulani. Kwa hivyo, kutokana na sababu walizozitoa, makosa huwa ni ya kiutendaji na vilevile husababishwa na kutozingatiwa kwa sheria za lugha husika. Hali kadhalika, inabainika kuwa makosa huweza kutokea katika lugha ya kwanza au hata katika lugha ya pili japo wazungumzaji asilia wa lugha fulani huwa na uwezo wa kutambua makosa punde tu yanapojitokeza.

Elis (1997) anasema kuwa, makosa husababishwa na kutozingatia sheria za lugha. Kadhalika, ameongezea kuwa, ikiwa mwanafunzi ana uwezo wa kukosoa kosa lake yeye binafsi, basi hilo ni jambo jepesi na halifai kushughulikiwa. Zaidi ya hayo, anasisitiza kwamba, ikiwa mzungumzaji ana uwezo wa kushughulikia matatizo yake katika lugha na kuzirekebisha vilivyo basi hali hiyo inaashiria kuwa mtumizi lugha ana umilisi wa lugha hiyo. Hali kadhalika, ikiwa mtumizi lugha hana uwezo huo wa kufanya hivyo basi hilo ni tatizo ambalo linafaa kushughulikiwa vilivyo kwa kuwa mzungumzaji hana umilisi wa lugha na hutambua sheria zozote za lugha husika.

Mtazamo wa Corder (Ibid) inashabihiana na wa Brown (Ibid), kwani wote wanakubaliana kuwa makosa katika lugha hujidhihirisha katika viwango vyote vya isimu. Japo, Brown (1987) amepiga hatua na kuongezea kuwa, makosa huweza kuhusu ulimwengu mzima au yaweza kuwa ya kimaeneo.

Corder (1973) kadhalika anasema kuwa makosa huweza kuwa wazi au yasiwe wazi. Makosa yaliyowazi aghalabu huwa ni ya kisarufi na hutambulika kwa urahisi katika kiwango cha sentensi. Kwa upande mwingine, makosa yasiyokuwa wazi huwa mara

nyingi huchukuliwa kuwa sahihi kisarufi bali maana ya sentensi hizo ndizo hazieleweki. Kwa mujibu wa Brown (1993) matatizo ya wanafunzi wanapojifunza lugha ya pili hutokea kwa kuwa wanafunzi hao hawatambui mfumo na kanuni za lugha husika. Kadhalika mtaalam huyo anasema, wanafunzi wengi hukosa ujuzi katika lugha ya pili kwa hivyo hawawezi kutambua makosa katika lugha hiyo. Aidha ameongezea kuwa matatizo katika lugha mara nyingi yana uzito na pia kudhihirika mwanafunzi anapotumia lugha.

Lennon akinukuliwa na Brown (2000) anasema, matatizo huweza kushughulikiwa kwa namna ifuatayo: kuanzia fonimu hadi semantiki na vilevile pragmatiki ambayo huchunguza maana kwa kuzingatia muktadha wa matumizi ya neno fulani.

Licha ya hayo, wataalam kama Richard (1974) na Selinker (1972) wameshughulikia swala hili na kuorodhesha aina nne za makosa katika tungo. Mathaalan,

- Uhamishaji lugha
- Ufundishaji mbaya wa lugha ya pili
- Mikakati ya kuwasiliana katika lugha ya pili
- Ujumlishaji mno wa kiholela

1.8.1 Uhamishaji lugha

Ni utaratibu wa kuhamisha kiambajengo cha lugha moja na kukitumia katika lugha nyingine. Wanafunzi wengi haswa huchukulia kuwa faridi za lugha ya kwanza na za lugha ya pili zinafanana. Vilevile, wanafunzi husadiki kuwa, kanuni zinazotawala lugha mbili ni mamoja kwa hivyo zinaweza kutumiwa katika lugha zote mbili kwa njia ya kubadilishana.

1.8.2 Ufundishaji mbaya wa lugha ya pili

Hali hii hutokana na ukosefu wa umilisi wa lugha ya pili. Walimu aghalabu hukosa mbinu mwafaka wanapofunza lugha ya pili. Licha ya hayo, walimu hukosa ujuzi toshelezi katika lugha kwa kuwa baadhi yao hutumia mbinu zisizofaa zikiwemo ujumlishaji wa kiholela na pia matumizi mabaya ya sheria za lugha husika.

1.8.3 Mikakati ya kuwasiliana katika lugha ya pili

Mawasiliano katika lugha ya pili hutokana na njia mahususi ambazo watu hujifunza ili kuweza kuwasiliana na wazungumzaji asilia wa lugha lengwa. Mara kadhaa, mwanafunzi hujaribu kadri awezavyo ili akabiliane na upungufu alionao katika lugha lengwa. Kwa sababu hiyo mwanafunzi huyo hujikakamua ili afikie mawasiliano bora iwezekanavyo.

1.8.4 Ujumlishaji mno wa kiholela

Ujumlishaji ni utoaji wa mahitimisho maelezo ya kijumla sana hadi kuvuka mpaka. Wanafunzi aghalabu hutumia sheria kiholela au hata pasipofaa. Kwa hivyo kutokana na harakati hizo, wanafunzi hubuni chukulizi kuhusu lugha lengwa na pia kuzitumia kanuni za lugha ya kwanza katika lugha ya pili. Hali hiyo hutatiza matumizi ya lugha ya pili na vilevile kusababisha makosa mengi katika lugha ya pili.

Kwa jumla, nadharia hii imekuwa na manufaa mengi katika utafiti huu kwa kuwa kupitia kwa nadharia hii tumeweza kubaini athari ya Kisuba kwenye Kiswahili sanifu. Aidha nadharia hii imetuwezesha kulinganisha mfumo wa lugha mbili mathaalan Kisuba na Kiswahili na hivyo kubaini tofauti zinazojitokeza baina ya lugha hizo mbili.

Kadhalika kwa kuwa nadharia hii ina uwezo wa kutambua chanzo cha makosa na pia kutabiri kutokea kwa makosa katika lugha ya pili, nadharia hii ilitufaa katika kazi hii kwa kuwa chanzo cha makosa mengi yalibainishwa na hatimaye makosa hayo kushughulikiwa ipasavyo.

Mbali na nadharia ya uchanganuzi linganuzi, nadharia ya sarufi mapokeo na sarufi miundo pia imetufaa katika utafiti huu. Nadharia ya sarufi miundo iliasisiwa na wanaisimu kama Franz Boaz, Edward Sapir, Leonard Bloomfield japo Ferdinand De Saussure (1857-1913) alichangia pakubwa katika nadharia hii. Mwanaisimu huyu alijadili dhana zifuatazo:

Uhusiano wima na uhusiano mlalo

Mfumo lugha na utendaji

Isimu Historia na Isimu mamboleo

Ishara ya Kiisimu

Uchanganuzi kiuambajengo

Ijapokuwa Ferdinand aliangazia dhana kadhaa katika nadharia hii, utafiti huu umetumia dhana moja tu ambayo ni uchanganuzi kiuambajengo. Kwa mujibu wa Mweri (2010), uchanganuzi kiuambajengo ni mbinu ya uchanganuzi wa sentensi ambayo hugawanya sentensi kwa kutumia dhana ya upanuzi. Dhana hii hujikita katika mfanano wa ruwaza. Kadhalika kigezo hiki huweka mpaka kati ya jina la mtenda na tendo. Zaidi ya hayo, uchanganuzi kiuambajengo hutumia dhana ya upanuzi unaobadilisha muundo mmoja na mwingine unaofanana nao katika mazingira sawa.

Licha ya hayo, nadharia ya sarufi mapokeo pia imetumiwa katika utafiti huu. Kitengo cha nadharia kilichotufaa zaidi kilikuwa uchanganuzi wa viambajengo vya sentensi.

Kulingana na kitengo hicho, sentensi huweza kuundwa kwa viambajengo vya viwango vya juu kama vikundi na vishazi au hata viambajengo vidogo kuliko sentensi. Kadhalika, wananadharia hii huchukulia kuwa, maneno tofauti hufanya kazi tofauti katika uundaji wa sentensi. Zaidi ya hayo, maneno huweza kuainishwa katika makundi tofauti kulingana na maana na utendaji kazi wake. Pamoja na hayo, nadharia hii vilevile huangazia aina mbalimbali za maneno ambayo huitwa kategoria za maneno.

Kwa jumla, nadharia ya sarufi mapokeo na sarufi muundo zimetufaa katika utafiti huu kwa kuwa kupitia kwa nadharia hizi, sentensi za Kisuba na Kiswahili zimeweza kuainishwa na mambo mengi kubainika kuhusu lugha hizo. Mathaalan, tumebaini sifa bainifu za sentensi za Kisuba na Kiswahili sanifu, na vilevile viambajengo vya sentensi hizo. Kadhalika uchanganuzi wa kiuambajengo wa sentensi pia umerahisishwa kupitia kwa nadharia ya sarufi mapokeo.

1.9 Mbinu za Utafiti

Sehemu hii imeeleza kwa jumla kuhusu ukusanyaji wa data na uchanganuzi wa data.

Katika ukusanyaji wa data, mahali kama nyanjani, maktaba zitakuwa nguzo kuu.

Uchanganuzi wa data ulitokana na uteuzi wa data na kisha uchanganuzi wa data hizo.

1.9.1 Ukusanyaji data

Ukusanyaji data hususan ulikuwa nyanjani. Wazungumzaji asilia wa lugha ya Kisuba walihojiwa ili kubaini baadhi ya sentensi na matamshi mwafaka wa maneno. Aidha Biblia ya Kisuba *Endagano Empia* pia ilichangia pakubwa katika kufanikisha kazi hii kwa kuwa maneno yalidondolewa kutoka humo na kuainishwa ipasavyo. Kadhalika kifaa kilichotumiwa katika uchanganuzi wa data kilikuwa baa grafu. Pamoja na hayo, shule ambayo ilihusishwa katika uandishi wa insha ilikuwa shule moja tu. Shule hiyo ilipendekezwa kwa kuwa wanafunzi wake hususan hutumia Kisuba wanapokuwa

nyumbani. Kwa hivyo kutokana na sababu hiyo, tunachukulia kuwa lugha yao ya kwanza ambayo ni Kisuba haijathiriwa pakubwa na lugha nyingine. Zaidi ya hayo, darasa ambalo lilihusishwa katika utafiti huu lilikuwa darasa la saba japo sio wanafunzi wote walihusishwa bali wale ambao waliteuliwa kwa misingi ifuatayo. Kwa kuwa darasa hilo lilikuwa na jumla ya wanafunzi thelathini na wawili idadi hiyo iliyokuwa kubwa mno, tuliteua wanafunzi kumi na sita ambayo ndiyo sampuli iliyowakilisha darasa zima. Mbinu iliyotumiwa ilikuwa ni kuwahoji wanafunzi wote kutoka darasani humo ili kubaini wale walio na uwezo wa kuzungumza Kisuba barabara na pia wale ambao wanatumia lugha hiyo nyumbani. Kwa kuwa idadi ya waliosalia bado ilikuwa kubwa, tuliandika majina yao kwenye vijikaratasi vidogo, tukavikunja vijikaratasi hivyo na kisha kuvitumbukiza kwenye kikapu. Tulivikoroga kwa muda wa sekunde thelatini, baadaye wanafunzi wa kwanza kumi na sita waliviokota vijikaratasi hivyo na kuvikunjua. Wale ambao majina yao yalikuwa kwenye vijikaratasi hivyo ndio walihusishwa katika uandishi wa insha.

1.9.2 Mahali pa utafiti

Utafiti huu ulifanywa kwenye kisiwa cha Mfangano kwa kuwa hapo ndipo Kisuba huzungumzwa sana. Aidha, shule ambayo ilihusishwa katika uandishi wa tungo ilikuwa shule ya msingi ya Nyahera. Shule hiyo ilipendekezwa kwa kuwa kati ya shule zote Mfangano, shule hiyo ndiyo shule ambayo wanafunzi wake huzungumza Kisuba bila tatizo lolote na pia wanafunzi hao hutumia lugha hiyo wanapokuwa nyumbani.

1.9.3 Mbinu ya utafiti

Mbinu iliyotumiwa katika kazi hii ilikuwa kusoma insha kwa madhumuni ya kuorodhesha kila aina ya kosa na kisha kuyashughulikia ipasavyo. Kadhalika, nilitumia ujuzi wangu wa lugha hii. Vilevile, Bibilia ya Kisuba ilikuwa muhimu katika utafiti huu kwa kuwa baadhi ya maneno yalitolewa humo. Wanafunzi pia walihusishwa katika uandishi wa insha. Pamoja na hayo, tuliwahoji wazee ili kubaini eneo ambalo Kisuba hakijaathiriwa pakubwa na lugha jirani na vilevile wazee hao walituelekeza kumtambua aliyekuwa na uwezo wa kuzungumza lugha ya Kisuba na Kiswahili barabara.

1.9.4 Uchanganuzi wa data

Baada ya kusahihisha insha za wanafunzi, makosa yaliorodheshwa na kuainishwa. Kwa kuwa kulikuwa na makosa mengi, mtafiti alidondoa yale makosa ya kisintaksia. Aidha sio makosa yote ya kisintaksia yalishughulikiwa bali yale yaliyosababibishwa na athari ya lugha ya kwanza pekee.

Kadhalika, uchanganuzi ulihusu kategoria za maneno katika tungo na ubainisho wa viambajengo. Zaidi ya hayo, mtafiti aliorodhesha sentensi kadhaa za Kisuba na Kiswahili kisha akazilinganisha na kuzilinganua sentensi hizo. Shughuli hii iliwezesha kubaini uhusiano uliopo kati ya lugha hizo mbili. Kadhalika, visababishi vya makosa viliorodheshwa na kisha kushughulikiwa vilivyo. Licha ya hayo sentensi kadhaa ziliainishwa ili kubaini zile ambazo wanafunzi hao walitoa mahitimisho maelezo ya kijumla sana hadi kuvuka mpaka. Shughuli hiyo yote ilichangia katika utambuzi wa makosa yanayohusishwa na tofauti kati ya lugha hizo mbili.

1.10 Hitimisho

Sura hii imejadili kwa kina usuli wa mada, swala la utafiti na pia madhumuni ya utafiti huu yameorodheshwa. Kadhalika, mwandishi ametaja kazi alizozipitia na vilevile kutaja namna kazi hizo zilinufaisha utafiti huu. Zaidi ya hayo, sehemu ya mwisho inahusu mbinu za utafiti ambapo mtafiti amefafanua kwa kina njia zinazostahili kumfaidi katika uchanganuzi wa data. Aidha katika kitengo hicho, mtafiti ametaja namna tungo kadhaa za wanafunzi zinafaa kushughulikiwa.

SURA YA PILI

UCHANGANUZI LINGANUZI WA SENTENSI ZA KISUBA NA KISWAHILI

SANIFU

2.0 Utangulizi

Sura hii imelinganisha sentensi za Kiswahili sanifu na za Kisuba ili kubaini tofauti zilizoko kati ya lugha hizo mbili. Ulinganuzi wa sentensi za Kisuba na Kiswahili umehusisha nadharia ya sarufi mapokeo na sarufi miundo. Nadharia hizi zimeangaziwa mno na Crystal (1971). Sura hii pia imechunguza dhana ya sintaksia haswa ikijikita kwenye kitengo cha sentensi. Vilevile, elementi kadhaa zimelinganishwa kwa undani. Elementi hizo ni pamoja na: nomino, vivumishi, viunganifu na vitenzi. Kadhalika sura hii, imejadili mpangilio wa maneno katika tungo na sheria zinazohusika katika uundaji wa sentensi.

Kipashio cha kiisimu cha sintaksia kimekuwa muhimu katika kazi hii kwa kuwa kitengo hicho hushughulikia uchanganuzi, mpangilio na uhusiano wa vipashio vinavyounda sentensi. Dhana hiyo pia hushughulikia muundo wa sentensi na elementi zinazounda sentensi. Aidha, kitengo hiki huhakiki mpangilio wa maneno yanayounda sentensi na vilevile kusesitiza utaratibu mwafaka wa sheria za uundaji wa sentensi zenye maana. Kwa mfano, katika sentensi za Kiswahili, nomino huja kabla ya kivumishi ilhali vielezi hutumiwa baada ya vitenzi. Kwa sababu hiyo, sio sahihi katika lugha ya Kiswahili kusema,

- 1 *Mrefu mtoto vibaya analia.
- 2.*Alienda mama sokoni jioni jana.
- 3.*Nguo mpya Amina amenunua.

Sentensi hizi zimekiuka sheria za utunzi wa sentensi. Fauka ya hayo, sura hii imejadili kategoria za maneno na muundo wa sentensi haswa sentensi sahili. Vilevile, sura hii imefafanua kwa kina sehemu za kimsingi za sentensi kama vile maneno ambayo aghalabu hujenga virai na kisha virai hivyo vikajenga vishazi na hatimaye sentensi kuundwa. Aidha katika kiwango cha sentensi kuna kiima na kiarifu. Sehemu hizi za sentensi zimejadiliwa kwa kina moja baada ya nyingine ili kutambua sifa zinazozifananisha na kuzitofautisha lugha za Kisuba na Kiswahili.

2.1 Viambajengo vinavyounda sentensi

Uchunguzi wa viambajengo hivi vimechangia katika kubainisha ikiwa kuna tofauti za kisintaksia baina ya sentensi sahili za Kiswahili sanifu na za Kisuba. Aidha uchunguzi wa viambajengo hivyo umefanikisha kubaini kiwango ambacho lugha ya Kisuba huathiri Kiswahili sanifu.

2.1.1 Nomino za Kisuba

Nomino ni neno linalotaja kitu, hali, dhana au tendo. Uchunguzi wa nomino katika ulinganisho wa lugha mbili ni muhimu kwa kuwa inawezesha kufanikisha kazi husika kwa namna ifuatayo. Nomino ni kipashio muhimu katika kazi fulani kwa kuwa, kama ilivyo ada ya lugha za Kibantu, nomino hutawala miundo ya maneno mengine katika sentensi. Muundo huu ndio hurejelewa kama upatanisho wa kisarufi. Muundo huo hutofautiana kulingana na lugha husika na pia nomino inayoashiriwa. Kadhalika, nomino husheheni viambishi ambavyo huwakilisha hali anuwai katika neno. Kwa sababu hiyo, matumizi mabaya ya viambishi hususan husababisha makosa katika Kiswahili sanifu. Kwa mfano, ngeli ya pili ya Kisuba ina nomino kama,

4. **omuti** – mti
5. **omusiri** – shamba

6. **omutwe**– kichwa

Kutokana na mifano hii, tunabaini kuwa maneno mengi ya Kisuba ambayo yana maana sawa na ya Kiswahili hupatikana katika ngeli tofauti. Aidha mfano mwingine unadhihirika katika ngeli ya tisa ya Kisuba mathalaan,

7.**entewe**– kiti

8.**emburi**– mbuzi

Kwa kawaida, katika Kiswahili sanifu, kiti huainishwa kisintaksia katika ngeli ya Ki-Vi, ilhali nomino mbuzi huainishwa katika ngeli ya A-WA. Kwa hivyo mwanafunzi kutoka Mfangano hukumbwa na tatizo la uteuzi wa vipashio faafu vya nomino hizi.

Mfano wa sentensi iliyo na tatizo hili la uteuzi wa vipashio ni kama ifuatayo,

9. ***Kiti** ameanguka akaharibika

Kwa hivyo, uainisho wa nomino ni muhimu katika sura hii kwa kuwa mara nyingi tungo nyingi husheheni nomino au kiwakilishi chake. Pia imebainika kuwa nomino huathiri vipashio vingi katika sentensi na vilevile aghalabu huathiri jinsi ambavyo vipashio huchukuana na hukubaliana katika sentensi.

Pamoja na hayo, swala la upatanisho wa kisarufi huwatatiza wanafunzi kwa kuwa, japo upatanisho hudhihirika katika sentensi za lugha hizi mbili, bado kuna mwelekeo kuwa asilimia kubwa ya wanafunzi kazi zao husheheni makosa mengi yanayohusu upatanisho wa kisarufi.

Mifano ya sentensi za Kisuba na Kiswahili sanifu zinazodhihirisha upatanisho wa kisarufi.

Kisuba	Kiswahili
Omwaala a gingra amazi	Msichana a mebeba maji.
Awaala w agingra amazi	Wasichana w amebeba maji.
Eriiso r ino r ionike	Jicho hili l imeharibika
Ekinu k ino k ionike	Kinu hiki k imeharibika
Ewinu w ino w ionike	Vinu hivi v imeharibika
Entikiri e no e gingra amazi	Punda huyu a mebeba maji
Entikiri z ino z igingra amazi	Punda huyu w amebeba maji
Olutare l uno l uanikire ekiduma	Mwamba huu u meanikwa mahindi
Amatare g ano g aonikire ewiduma	Miamba hii i meanikwa mahindi
Omuti g uno g uzakukengwa	Mti huu u takatwa
Emiti g ino g izakukengwa	Miti hii i takatwa
Owusara w uno w uvulugwe geeza	Uji huu u mekorogwa vizuri
O kumenya ano k undongre	Ku ishi huku k umenisinya
A kamori k ano k arire owusuwi	Kibuzi hiki k imekula nyasi

Kutokana na jedwali hili, tunabaini kuwa, nomino ni kiungo muhimu iliyo na uwezo wa kuelekeza muundo unaochukuliwa na maneno mengine katika sentensi na huo ndio hurejelewa na wataalam wengi kama upatanisho wa kisarufi. Upatanisho hudhihirisha uhusiano wa kisintaksia ambapo neno moja hutawala umbo la kimofolojia la neno au maneno mengine katika tungo.

Aidha, japo waandishi wengi wamependekeza kuwa uainisho wa nomino kimofolojia ni mwafaka, utafiti huu unabaini kuwa una dosari kwa kuwa bado kuna nomino ambazo

matumizi yao yanakanganya kwa mfano nomino ‘**kiboko**’ na ‘**kipofu**’ miongoni mwa nomino nyingine. Matumizi ya nomino hizi katika tungo husababisha utata mwingi kwa kuwa majina yote yaliyo na kiambishi awali ‘ki’ katika Kiswahili huchukuliwa kuwa yanafaa kuainishwa katika ngeli ya KI-VI.

Kutokana na sababu hiyo, sio sahihi kusema,

10.*Kipofu kilianguka kikaumia

Kadhalika hali inayoshabihiana na hii inadhihirika katika Kisuba vilevile, kwa mfano, nomino

11.‘**Omuntu**’ yenye maana mbili: yaani

-mtu

-kiti.

Kutokana na hali hiyo, nomino ‘*omuntu*’ huweza kuainishwa katika ngeli ya kwanza na vilevile katika ngeli ya tatu kutegemea kiashiriwa. Kwa sababu hiyo, ili kuweza kutatua tatizo hili, ni vyema kutumia mfumo wa uainisho ulio na uwezo wa kuondoa utata miongoni mwa watumizi wa lugha na wanafunzi wakiwemo.

Hali kadhalika Kisuba kama ilivyo lugha ya Kiswahili hupanga nomino zake katika makundi yanayoitwa ngeli. Mpangilio huo hutumia viambishi vinavyowakilisha umoja na wingi na vilevile kutambulisha nomino katika ngeli husika. Mathaalan,

2.1.2 Jedwali linaloashiria Ngeli za Kisuba na za Kiswahili.

		Kisuba		Kiswahili sanifu
1	Ngeli za Kisuba	Nomino za Kisuba	Ngeli za Kiswahili	Nomino za Kiswahili sanifu
	Omu -	omugerezi,	a-	mwalimu, mkulima, mchawi

	/ Omw -	omurimi, omulozi omufugi, omwaana, omwaala		mfugaji, mtoto, msichana
2	Awa -	Awagerezi, awarimi, awalozi, awafugi, awaana, awaala	wa	Walimu, wakulima, warogi, wafugaji, watoto, wasichana
3	Omu - /Omi	Omuti, omioyo, omusiri, omutwe	mu-	Mti, moyo, shamba, kichwa
	Ogu -	Ogugombe, oguuzi, ogubwa, oguntu,	mu-	Gombe, buzi, jibwa, jitu
4	Emi -	Emiti, emioyo, emusiri, emitwe	mi	Miti, mioyo, mashamba, kichwa
5	Eri -/i-	Eriiso, eriina, igi, ingana, itoke, igosi, isaka, igondi	ji-	Jicho, jina, yai, neno, ndizi, shingo, kichaka, kondoo
6	Ama-	Amiiso,	ma	Macho, majina, mayai,

		amiina, amagi, amangana, amatoke, amagosi		maneno, ndizi, shingo
7	Eki –, Aka	Ekitabu, ekinu, ekirato, ekikapu Akantu , akabwa	ki-	Kitabu, kinu, kiatu, kikapu Kijitu, kijibwa
8	Ewi -	Ewitabu, ewinu, ewirato, ewikapu	vi	Vitabu, vinu, vyatu, vikapu
9	En -	Entewe, entikiri, emburi	-	Kiti, punda, mbuzi
10	Olu -	Oluvwiri, oluwago, olutare	u-zi	nywele, ua, mwamba
11	Owu -	Owusara, owusuwi	u-	Uji, nyasi
	Owi -	Owiita, uwiwi	u	Ugali, ubaya
12	Oku -	Okumenya, okusemera,	ku-ku	Kuishi, kutapika
13	Ku, mu	Muchiro, musukuli, Muhekalu, munyumba,	PA-KU- MU	Sokoni, shuleni, Hekaluni, nyumbani

		kunyumba		
--	--	----------	--	--

Kupitia kwa jedwali hili, tunabaini kuwa Kisuba na Kiswahili sanifu huainisha nomino zao katika makundi yanayoitwa ngeli. Japo uainisho huo unashabihiana katika lugha zote mbili, kunazo baadhi ya vipengele ambavyo vinatofautisha lugha hizo kama vile, maneno mengi ya Kisuba ambayo yana maana sawa na ya Kiswahili hupatikana katika ngeli tofauti.

Licha ya hayo, viambishi vya nomino pia huweza kuwakilisha dhana kadhaa katika sentensi husika.

2.1.3 Mifano ya viambishi vya nomino

<i>Kisuba</i>	<i>Kiswahili</i>
i) Omu-ti	m- ti
ii) Emi-ti	mi -ti
iii) Omwa-ala	m -sichana
iv) Awa-ala	wa- sichana
v) En-tewe	ki- ti

Kupitia kwa mifano hiyo, tunabaini kuwa nomino za Kisuba zina mofu ‘**omu-**’, ‘**emi-**’, ‘**en-**’ na ‘**om**’ ilhali nomino za Kiswahili zina mofu ‘**m**’, ‘**mi**’, ‘**ki**’, na ‘**m**’ ambavyo ni viambishi awali vya nomino za Kiswahili sanifu. Kadhalika, katika lugha zote mbili, imebainika kuwa, viambishi hivyo huwakilisha idadi ya nomino husika. Mathaalan, kiambishi ‘**omu-**’ katika Kisuba na kiambishi ‘**m**’ katika Kiswahili vinavyowakilisha hali ya umoja katika nomino ‘**omuti**’ na ‘**mti**’. Aidha, viambishi ‘**emi**’ na ‘**mi**’ katika nomino ya (ii) huwakilisha hali ya wingi wa nomino ‘**miti**’ na ‘**emiti**’.

Pamoja na hayo, ni muhimu kubaini kuwa mofu za Kisuba na za Kiswahili ni tegemezi. Mofu hizi sharti zitegemee mofu nyingine katika neno kwani haziwezi kujisimamia ili kuunda neno lenye maana. Kutokana na sababu hiyo, nyingi kati ya nomino na vivumishi vya lugha za Bantu, Kisuba kikiwemo, huundwa kwa mzizi tegemezi. Pamoja na hayo, ni dhahiri kuwa viambishi vyovyote ni mofu tegemezi katika lugha zote mbili.

2.1.4 Uainishaji wa nomino kisintaksia

Kama ilivyodokezwa hapo awali, uainishaji wa nomino kisintaksia una manufaa mengi ikilinganishwa na uainishaji wa kimofolojia kwa sababu uainishaji wa kisintaksia hutilia mkazo zaidi suala zima la uamilifu badala ya umbo au muundo wa nomino husika. Obuchi na Mukhwana (2010) wamesisitiza hoja hii. Aidha katika uainishaji wa ngeli kisintaksia, nomino ndizo hutawala viambishi vyote vinavyotumiwa katika tungo. Pamoja na hayo, kigezo cha uainishaji wa kisintaksia hupanga majina yaliyo na mianzo tofauti pamoja kwa kufuata mantiki ya upatanisho wa kisarufi. Vilevile, uainishaji wa kisintaksia huziainisha ngeli za nomino kwa kuzingatia uhusiano wa nomino na maneno mengine katika tungo. Uainishaji huu hutumia vipatanishi vya nomino. Vipatanisho kulingana na utafiti huu ni maumbo maalum ambayo huwekwa katika maneno mengine wakati nomino fulani inapozungumziwa. Vipatanishi hivi hupachikwa hasaa kwenye vitenzi, vivumishi na viwakilishi.

2.1.5 Jedwali la vipatanishi vya Kisuba na Kiswahili sanifu

Namba ri ya ngeli	Kipatanis hi cha Kisuba	Sentensi za Kisuba	Nambar i ya ngeli	Kipatanis hi cha Kiswahili	Sentensi za Kiswahili.
1	a-	Omwana omulootu agwiire aasi.	1	a-	Mtoto mzuri ameanguka chini
2	wa-	Awaana awalootu wagwiire asi	2	wa	Watoto wazuri wameanguka chini
3	gu-	Omuti guno guzakukengwa	3	u-	Mti huu utakatwa
	gi	Emiti gino gizakukengwa		i	Miti hii itakatwa
4.		Emitwe gikomoga ukalu			Vichwa vinatugonga sana
	ri-	Eriiso riange rionike	4.	li-	Jicho langu limeharibika
5.	ga	Amiiso giifu gaonike	5.	ya	Macho yangu yameharibika
6.		Gano na amiina ago Nyakiamo			Haya ni majina ya Nyakiamo
	ki-	Ekirato kiange ne	6.	ki-	Kiatu changu ni

		kilootu			kizuri
	wi-	Ewirato wiange ne wilootu		vi	Viatu vyangu ni vizuri
7.	e-	Entewe eno eonike uwiwi	7.	-	Kiti hiki kimeharibik a vibaya
8.	zi-	Entewe zino zionike uwiwi	8.	-	Viti hivi vimeharibik a vibaya
		Epunda zino zisingra amazi		-	Punda hawa wamebeba maji.
9.	lu-	Olutare luno luanikire ewiduma	9.	u-	Mwamba huu umeanikiwa mahindi
10.	wu-	Afumre owiita wuwisi ukalu	10.	u-	Ampika ugali uliombichi kabisa
11.	wu-	Owusara wuno wuvulugwe geza	11.	u-	Uji huu umekorogwa vizuri
	ku-	Okumenya ano kundongre		ku-	Kuishi huku kumenisinya
12.	Mu-	Gukwa aingire munyumba	12.	Mu-	Nyanya ameingia nyumbani.

13.	Mu-	Awagukwa waingire munyumba	13.	Mu-	Kina nyanya wameingia nyumbani.
-----	-----	---	-----	-----	---------------------------------------

Mifano ya sentensi zinazoashiria vipatanishi vya Kisuba na Kiswahili sanifu

Kisuba	Kiswahili
Owusara wuno wu vulugwe geza	Uji huu umekorogwa vizuri
Olutare luno lu anikire ewiduma	Mwamba huu umeanikiwa mahindi
Awaana walootu wag wiire aasi	Watoto wazuri wameanguka chini
Entewe zino zio nike uwiwi	Viti hivi vimeharibika vibaya
Emiti gino giz akukengwa	Miti hii itakatwa
Eriiso riange rion ike	Jicho langu limeharibika

2.1.6 Vipatanisho vya Kiswahili sanifu na za Kisuba

<i>Ngeli za kisuba</i>	<i>Ngeli za Kiswahili</i>	<i>Vipatanisho vya Kisuba</i>	<i>Vipatanisho vya Kiswahili</i>
Omu -, omwa	a-	(a-)	(a-)
awa -	wa-	(wa-)	(wa-)
omu-, ogu-	u-	(gu-)	(u-)
emi-	i-	(gi-)	(i-)
eri-	li-	(ri-)	(li-)
ami-, ama	ya-	(ga-)	(ya-)
eki-	ki-	(ki-)	(ki-)
ewi-	vi	(wi-)	(vi-)
en-	i-	(e-)	(i-)
zi-	zi	(zi-)	(zi-)
Olu-	u-u	(lu-)	(u-)

ama-	ya	(ga-)	(ya-)
owu-	Wu-	(wu-)	(u-)
owu-	wu	(wu)	(u-)
oku -	ku-ku	(ku)	(Ku-)
Pa-ku-mu		Pakumu	

2.2 Vivumishi

Vivumishi ni neno au maneno ambayo hufafanua kitu, sifa, hali au tendo

linalowakilishwa na nomino. Uchambuzi wa vivumishi ni muhimu katika kazi hii kwa kuwa wakati mwingi vivumishi hivyo hutumiwa kwa namna isiyo sahihi. Katika utafiti huu, vivumishi vilivyofafanuliwa kwa kina ni chache mno ijapokuwa kuna aina nyingi ya vivumishi. Vivumishi hivyo ni pamoja na, vivumishi vionyeshi vivumishi vya sifa, vivumishi vya idadi visivyo dhahiri, miongoni mwa vivumishi vingine.

2.2.1 Vivumishi vya -a unganifu

Hivi ni vivumishi ambavyo huundwa kwa kiambishi tamati -a. Kiunganifu -a ni aina ya kiambishi tamati kinachoambatanishwa kwenye kiambishi ngeli kwa ajili ya kuleta maana iliyokusudiwa kwenye upatanisho wa kisarufi baina ya makundi mbalimbali ya maneno.

2.2.2 Muundo wa viunganifu (-a) ni kama ifuatayo

Ngeli za kisuba	Kiunganifu -a za Kisuba	Ngeli za kiswahili	Kiungafu -a za kiswahili
Omu- Omwa-	wa	a-	wa
Awa-	wa	wa-	wa
Omu-/	gwa	mu-	wa

Omw-/ Ogu-			
Emi-	gya	mi-	ya
Eri	erio	ji-	la
Ama-/ Ami-	ago	ma-	ya
Eki-	ekia	ki-	cha
Ewi-	ewia	vi-	vi
En-	ezia	zi-	za
Owu-	owa	u-	wa

2.2.3 Matumizi ya kiunganifu (-a) katika sentensi za Kisuba na Kiswahili sanifu

Kisuba	Kiswahili
Ono no omwana wa senge	Huyu ni mtoto wa shangazi
Omuti guno no gwa gukwa	Mti huu ni wa nyanya
Rino ne eriina eria Nyakiamo	Hili ni jina la Nyakiamo
Gano na amiina ago Nyakiamo	Haya ni majina ya Nyakiamo
Ekikapu kino ne ekia gukwa	Kikapu hiki ni cha nyanya
Ewikapu wino no ewia gukwa	Vikapu hivi ni vya nyanya
Eno ne entewe eya omugerezi	Hiki ni kiti cha mwalimu
Zino ne entewe ezia awagerezi	Hivi ni viti vya walimu

Kupitia kwa jedwali hili tunabaini kuwa Kisuba na Kiswahili hutumia kiunganifu –a kwa namna inayoshabihiana. Kadhalika katika lugha zote mbili, kiunganifu –a hujitokeza kama kiambishi tamati kinachoambatanishwa kwenye kiambishi ngeli kwa ajili ya kuleta

maana iliyokusudiwa kwenye upatanisho wa kisarufi baina ya makundi ya maneno mbalimbali.

2.2.4 Vivumishi vionyeshi

Vivumishi vionyeshi huweza kuwa viwakilishi au vivumishi. Habwe na Karanja (2004) wametofautisha viwakilishi na vivumishi. Waandishi hawa wanasema, vivumishi husimama pamoja na nomino ilhali viwakilishi husimama pekee. Vivumishi vionyeshi huweza kuwa katika nafsi tatu kutegemea upatanisho wa ngeli. Vivumishi hivi huonyesha dhahiri kinachozungumziwa mathaalani, ni nani au nini kafanya jambo gani. Mfano katika sentensi,

12. Ng'ombe huyu ni mkali.

Katika sentensi hii kwa mfano, msemaji anatambulisha ng'ombe haswa aliyekuwa mkali na wala si ng'ombe yeyote.

Vivumishi vionyeshi hujidhihirisha katika lugha za Kiswahili na Kisuba kwa mfano, Kiswahili kina vivumishi vionyeshi vya namna tatu, yaani vivumishi vionyeshi vya karibu na msemaji, vivumishi vionyeshi vya karibu na msikilizaji, kadhalika kuna vivumishi vionyeshi visivyokuwa karibu na msemaji wala msikilizaji. Kwa upande mwingine, Kisuba kinasheheni vivumishi vionyeshi vya namna mbili pekee. Mathaalan, vivumishi vionyeshi vya karibu na msemaji na kadhalika vivumishi vionyeshi vya karibu na msikilizaji. Kwa hivyo, inadhihirika kuwa vivumishi vionyeshi vya Kisuba na Kiswahili vinatofautiana.

2.2.5 Vivumishi vionyeshi katika ngeli za Kisuba na za Kiswahili sanifu

Ngeli za Kisuba	Ngeli za Kiswahili	Kivumishi kionyeshi cha karibu na msemaji(Kisuba)	Kivumishi hi kionyeshi cha karibu na msemaji (Kiswahili)	Kivumishi shi kionyeshi cha karibu na msikilizi (Kisuba)	Kivumishi hi kionyeshi cha karibu na msikilizi (Kiswahili)	Kivumishi hi kionyeshi kisichokuwa karibu na msemaji wala msikilizi (Kisuba)	Kivumishi hi kionyeshi kisichokuwa karibu na msemaji wala msikilizi (Kiswahili)
A-	A-	Ono	Huyu	Aria	Huyo	-	Yule
Wa-	Wa-	Wano	Hawa	waria	Hao	-	Wale
Gu-	U-	Guno	Huu	Guria	Huo	-	Ule
Gi-	I-	Gino	Hii	Garia	Hiyo	-	Ile
Ri-	Li-	Rino	Hili	Riria	Hilo	-	Lile
Ga-	Ya-	Gano	Haya	Garia	Hayo	-	Yale
Eki-	Ki-	Kino	Hiki	Kiria	Hicho	-	Kile
Ewi-	Vi-	Wino	Hivi	Wiria	Hivyo	-	Vile
En-	I-	Eno	Hii	Eria	Hiyo	-	Ile
Zi-	Zi-	Zino	Hizi	Ziria	Hizo	-	Zile
Olu-	U-	Luno	Huu	Luria	Huo	-	Ule
Wu-	U-U	Wuno	Huu	Wuria	Huo	-	Ule

2.2.6 Mifano ya matumizi ya vivumishi vionyeshi katika sentensi

Kisuba	Kiswahili sanifu
Omuti guno gukeurwe	Mti huu umekatwa
Omuti guria gukeurwe	Mti huo umekatwa
Emuti giria gukeurwe	Miti hiyo umekatwa
Igondi rino ritekre kumwai	Kondoo huyu amempotelea mchungaji
Igondi riria ritekre kumwai	Kondoo huyo amempotelea mchungaji

Aidha kupitia kwa jedwali hili, ni wazi kuwa vivumishi vionyeshi vya lugha zote mbili vina sifa zinazofanana. Kwa mfano, mzizi wa kivumishi na mofu zinawakilisha kipatanishi cha nomino inayoashiriwa. Pamoja na hayo, viashiria hivi pia huashiria hali mbalimbali kutegemea ngeli husika.

2.2.7 Mifano ya vivumishi vionyeshi katika jedwali.

Kisuba	Kiswahili	Kisuba	Kiswahili
umoja	umoja	wingi	wingi
Omwana ono	Mtoto huyu	Awaana wano	Watoto hawa
Omuti guno	Mti huu	Emiti gino	Miti hii
Emeza eno	Meza hii	Emeza zino	Meza hizi
Igi rino	Yai hili	Amagi gano	Mayai haya
Itoke rino	Ndizi hii	Amatoke gano	Ndizi hizi

2.2.8 Vivumishi vya sifa

Vivumishi hivi hueleza sifa ya nomino inayovumishwa. Mbali na hayo, vivumishi vya sifa huchukua viambishi vya ngeli ilhali baadhi yao havichukui viambishi hivyo kwa mfano vivumishi vya mkopo kama, **safi, dhaifu** na **nadhifu**

Kadhalika, katika Kisuba na Kiswahili, mofolojia ya vivumishi hivyo vina sehemu kuu mbili yaani, kiambishi awali cha kivumishi ambacho hufanana na kiambishi awali cha nomino inayovumishwa. Vilevile, mzizi wa vivumishi hivyo aghalabu hubeba maana ya kileksika ya vivumishi hivyo.

2.2.8.1 Mifano ya sentensi zinazosheheni vivumishi vya sifa

Kisuba	Kiswahili
Omwana omulootu agwiire aasi.	Mtoto mzuri ameanguka chini.
Emiti gino emilootu gikeurue.	Miti hii mizuri imekatwa.
Irino riange ne ilootu ikalu.	Jina langu ni zuri sana.
Ewirato wiange ne ewilootu .	Vyatu vyangu ni vizuri .
Entikiri eno ndootu egingra amazi.	Punda huyu mzuri amebeba maji.
Amiino gifu no amalootu .	Meno yetu ni mazuri .

Kutokana na jedwali hili tunabaini kuwa viambishi awali vya vivumishi vya sifa vya Kisuba na Kiswahili vinafanana na viambishi awali vya nomino inayovumishwa. Pia katika lugha hizo mbili, mzizi wa kivumishi (**-zuri**) na (**-ootu**) ndiyo hubeba maana ya kileksika ya vivumishi hivi. Kwa hivyo, kulingana na ufafanuzi huu, mzizi (**-zuri**) katika lugha ya Kiswahili na (**-ootu**) katika Kisuba, huambishwa kwa namna tofauti kutegemea nomino inayovumishwa.

2.2.8.2 Mifano ya vivumishi vya sifa kwa kurejelea ngeli tofauti za Kisuba na Kiswahili sanifu

<i>NgeliKisuba</i>	<i>Ngeli za Kiswahili</i>	<i>Kivumishi cha sifa chenye mzizi (-lootu)</i>	<i>Kivumishi cha sifa chenye mzizi (-zuri)</i>
a-wa	a-wa	Omulootu Awalootu	Mzuri Wazuri
Gu-gi	u-i	Omulootu Emilootu	Mzuri Mizuri
Ri-ga	li-ya	Ilootu Amalootu	Zuri Mazuri
Ki-wi	Ki-vi	Kilootu Wilootu	Kizuri Vizuri
E-zi	i-zi	Ndootu Ndootu	Nzuri Nzuri
Wu-	u-u	walootu	Mzuri
Ku-	Ku-ku	Kulootu	Kuzuri
Mu- ku	Pa-ku-mu	Mulootu Kulootu	Pazuri Kuzuri

Mifano ya sentensi zinazoshiria matumizi ya vivumishi vya sifa

Kisuba	Kiswahili
Ewirato wino ne ewilootu	Viatu hivi ni vizuri
Emiti gino emilootu gikeurue	Miti mizuri imekatwa
Amiino gano ne amalootu	Meno haya ni mazuri
Iriina riange ne ilootu	Jina langu ni zuri
Entikiri eno ndootu egingra amazi amaji	Punda huyu mzuri amebeba maji

2.2.9 Vivumishi vya idadi visivyodhahiri

Vivumishi hivi hutaja kiasi fulani cha idadi kwa ujumla bila kujikita kwenye idadi mahususi. Pamoja na hayo, ni muhimu kuzingatiwa kuwa, vivumishi vina sehemu kuu mbili yaani kiambishi awali ambacho pia ni kipatanishi cha nomino kinachowekwa kabla ya mzizi wa kivumishi. Aidha, vivumishi hivyo vilevile husheheni mzizi.

Katika sura hii, vivumishi vya idadi visivyodhahiri vilivyochunguzwa katika kazi hii ni vivumishi vyenye mzizi *-ingine* na *-ote*.

Mofu *-ingine* hubeba maana tofauti kwa kutegemea muktadha wa matumizi yake. Pia mofu hii ina maana tatu ambazo ni ‘sehemu ya’ ‘baadhi ya’ na ‘zaidi ya’. Hali kadhalika, aina hii ya mofu huonyesha vitu vilivyojitenga na kundi la vitu vinavyofanana. Kwa mfano katika sentensi,

13. Ng’ombe **wengine** walichinjwa.

Sentensi hii ina maana kuwa, katika kundi fulani mahususi la ng’ombe, kuna sehemu ambalo lilichinjwa na sehemu ambalo halikuchinjwa.

2.2.9.1 Mofu (*-ingine*) huweza kujidhihirisha kwa namna zifuatazo katika lugha zote mbili

	<i>Ngeli za kisuba</i>	<i>Ngeli za kiswahili</i>	<i>Kisuba</i>	<i>Kiswahili sanifu</i>
1&2	a-wa	a-wa	Awana wandi waazre wano.	Watoto wengine walikuja hapa.
3&4	gu-gi	u-i	Emiti giindi gikengrwe.	Miti mingine ilikatwa
5&6	ri-ga	li-ya	Amiina gandi gawulano.	Majina mengine hayapo
7&8	ki-wi	ki-vi	Ewirato wiindi wiwulano.	Viatu vingine havipo.
9&10	e-zi	i-zi	Entewe ziindi ezia omugerezi ziwulano.	Viti vingine vya mwalimu havipo.
11&12	Olu-	u-zi	Emvwiri ziindi zisukrwe geza.	Nywele zingine zimesukwa vizuri.

13&14	Wu	u-u	Owiita undi uwulano ano.	Ugali mwingine haupo hapa.
-------	----	-----	---------------------------------	-----------------------------------

Kupitia kwa jedwali hili tunabiani kuwa vivumishi hivi vina sehemu kuu mbili ambavyo ni kiambishi awali na mzizi.

Aidha katika ngeli ya pili, kiambishi awali cha kivumishi hicho ni ‘**wa**’ katika lugha zote mbili ilhali mizizi ya vivumishi hivyo ni ‘**-ndi**’ katika Kisuba na ‘**-ngine**’ katika Kiswahili sanifu. Kadhalika, viambishi hivyo aghalabu ni kipatanishi cha wingi cha nomino na hutumika kabla ya mzizi wa vivumishi.

2.2.9.2 Mifano ya sentensi zinazodhihirisha matumizi ya mofu –ote /-ona)

Ngeli za Kisuba	Kisuba	Ngeli za kiswahili	Kiswahili
a-wa	Awatu woona wazire	a-wa	Watu wote walikuja
gu-gi	Emiti giona gizakukengwa	u-i	Miti yote itakatwa
ri-ga	Amiino goona gaonike	li-ya	Meno yote yameharibika
ki-wi	Ewirato woona wilootu wionike	Ki-vi	Viatu vyote vizuri vimeharibika
e-zi	Entewe ziona awageni wikaale	i-zi	Viti vyote wageni wamekalia
lu-	Emvwiri ziona zisukrwe geza	u-zi	Nywele zote zilisukwa vizuri
wu-	Omwana ono ariire owiita wuona	u-u	Mtoto huyu amekula ugali wote

2.3 Viwakilishi

Kwa mujibu wa Mgullu (1999), viwakilishi ni maneno ambayo hutumiwa badala ya nomino. Maneno haya huziwakilisha nomino na ndiyo maana yakaitwa viwakilishi. Viwakilishi vinapotumika, nomino zinazowakilishwa na viwakilishi hivyo huwa hazitajwi. Kimofolojia viwakilishi hufanana na vivumishi isipokuwa vile viwakilishi vya nafsi. Kadhalika, ijapokuwa kuna viwakilishi vingi, utafiti huu umeshughulikia chache mno haswa vile ambavyo matumizi yao hutatiza wanafunzi.

2.3.1 Viwakilishi vya nafsi

Kwa mujibu wa Mgullu (1999) viwakilishi vya nafsi ni viwakilishi ambavyo hukaa badala ya majina ya watu. Viwakilishi hivi vimegawanywa katika nafsi tatu kuu, yaani, nafsi ya kwanza ambayo huhusu mtu anapozungumza habari zake mwenyewe au watu wanapozungumza habari zao wenyewe. Aidha nafsi ya pili huhusu unayezungumza naye, naye anakusikiliza na wewe unayezungumza unamweleza anayesikiliza habari zake. Kadhalika, nafsi ya tatu huhusu mtu au watu mnaozungumza habari zao lakini wao hawapo katika mazungumzo hayo. Kwa hivyo, vipo viwakilishi vya nafsi vya aina tatu. Mathaalan, nafsi ya kwanza, nafsi ya pili na nafsi ya tatu.

2.3.2 Jedwali la viwakilishi nafsi

Nafsi	Kisuba	Kiswahili
Nafsi ya kwanza		
umoja	Inze	Mimi
Wingi	Ifue	Sisi
Nafsi ya pili		
Umoja	Iwue	Wewe
Wingi	Inywe	Nyinyi

Nafsi ya tatu		
Umoja	Iyie	Yeye
Wingi	Iwo	Wao

Kisuba na Kiswahili sanifu husheheni viwakilishi. Viwakilishi hivyo huashiria nafsi mbalimbali katika umoja na pia katika wingi. Viwakilishi hivi katika lugha mbili huweza kutumiwa badala ya nomino. Kwa mfano,

Kiswahili: Yeye amekuja

Kisuba: Iyie aazira

2.4 Vitenzi

Kitenzi ni neno linaloeleza jambo linalofanyika. Aidha vitenzi hutoa taarifa, maswali au amri. Pamoja na hayo, vitenzi vinatekeleza majukumu mengi katika sarufi kwa mfano, vitenzi hubeba viambishi vipatanishi vinavyoashiria hali ya upatanisho. Pamoja na hayo, vitenzi vya lugha za Bantu aghalabu hufungiliwa viambishi mbalimbali kwa mfano,

14.Ni-na-ruk-a.

Kitenzi hiki kina viambishi kama,

'ni' ambayo huwakilisha nafsi

Ilhali **'na'** ikirejelea njeo

na **'ruk'** ndiyo mzizi wa kitenzi.

ani kiishio

Uchunguzi wa vitenzi katika kazi hii ni muhimu kwa kuwa mbali na viambishi vilivyotajwa, swala la upatanisho wa kisarufi pia hudhihirika katika vitenzi vya lugha za Kiswahili na Kisuba. Pamoja na hayo, imebainika kuwa vitenzi huathiriwa na vipengele vingi vya sentensi .Kwa mfano, nomino huamua kipatanisho kinachostahili kutumiwa

katika sentensi. Vipatanisho hivyo aghalabu hupachikwa kwenye vivumishi na viwakilishi.

Kwa mfano,

Kisuba	Kiswahili
entewe zino zionike uwiwi	viti hivi vimeharibika vibaya

Kutokana na mfano huu, ‘**zi**’ huwakilisha kipatanishi cha kisarufi katika Kisuba ilhali ‘**vi**’ huwakilisha kipatanishi katika Kiswahili sanifu.

Kadhalika vitenzi huweza kukaa pekee kama sentensi bila kusaidiwa na maneno mengine.

Kwa mfano,

Kiswahili	Kisuba
amekuja	aziira

Vilevile, kutokana na utafiti huu, tumebaini kuwa vitenzi vya Kisuba aidha huweza kuambishwa viambishi kadhaa,

Kwa mfano,

15. ‘**A-zaoku-rim-a**’ (yenye maana atalima)

Neno hili lina mofu kadhaa. Mathaalan

Mofu ‘**a-**’ inayoashiria nafsi na vile vile inawakilisha hali ya umoja

Mofu ‘**-zaoku**’ inaashiria wakati ujao.

Mofu ‘**-rim**’ inaashiria mzizi wa kitenzi hiki.

Mofu ‘**-a**’ inayoashiria kiishio

Mfano kama huu unaodhihirika katika lugha ya Kiswahili kwa mfano, kitenzi atalima inasheheni mofu zifuatazo

Mofu ‘**a-**’ inawakilisha nafsi, na pia hali ya umoja

Mofu ‘**ta**’ – inaashiria wakati ujao

Mofu’ **lim-** inayoashiria mzizi wa kitenzi

Mofu ‘**-a**’ inayoashiria kiishio

Lugha hizi pia kama ilivyo ada ya lugha za Kibantu zinasheheni ruwaza ya kiarifu kutanguliwa na kiima .Mifano hiyo inajitokeza katika baadhi ya sentensi za Kisuba na Kiswahili sanifu.

2.4.1 Sentensi zinazosheheni viarifu vya Kisuba na Kiswahili sanifu

Kisuba	Kiswahili sanifu
Awaana waria ipapai	Watoto wanakula papai
Ekikere kidumaduma	Chura anarukaruka .
Awaana wanoga esaafu kuomuti	Watoto wanachuma matunda mitini
Awaala wagonzizie okuiwaka amavuta	Wasichana wanapenda kujipaka mafuta
Katonda amenyere kuegulu	Mungu anaishi mbinguni
Olutare luno luanikire ewiduma	Mwamba huu umeanikwa mahindi
Amatare gano gaonikire ewiduma	Miamba hii imeanikwa mahindi
Omuti guno guzakukengwa	Mti huu utakatwa
Owusara wuno wuvulugwe geza	Uji huu umekorogwa vizuri
Okumenya hano kudongre	Kuishi huku kumenisinya
Akamori ano akawiwi karire ewiduma	Kibuzi hiki kibaya kimekula mahindi
Ewimori wino ewiwi wirire ewiduma	Vibuzi hivi vibaya vimekula mahindi

‘**Waria ipapai**’, ‘**kidumaduma**’, ‘**wanoga esaafu kuomuti**’, ‘**wagonzizie okuiwaka amavuta**’ na ‘**amenyere kuegulu**’ pamoja na viarifu vingine ndivyo vilivyotanguliwa

na kiima katika Kisuba. Vilevile katika Kiswahili sanifu ‘wanakula paipai’, ‘anarukaruka’, ‘wanachuma maua mitini’, ‘wanapenda kujipa mafuta’, na ‘anayeishi’ ndivyo baadhi ya viarifu vya sentensi hizo. Aidha, maswala kadha pia huweza kujitokeza katika vitenzi. Kwa mfano,

2.4. 2 Vikanushi vya vitenzi vya Kisuba na Kiswahili

Kisuba	Kisuba hali ya kukanusha	Kiswahili	Kiswahili hali ya kukanusha
Nyemba	Ng’anyemba	Ninaimba	Siimbi
Galuka	Ng’agaluka	Ninaruka	Siruki
Jojia	Ng’ajojia	Ninaandika	Siandiki
Fumba	Ng’afumba	Ninapika	Sipiki
Mugonzizie	Ng’amugonzizie	Ninampa	Simpi
Nyozia	Ng’anyozia	Ninafua	Sifui
Tuemba	Ng’atuemba	Tunaimba	Hatuimbi

Kiambishi awali ‘*ng’a*’ katika vitenzi ‘ng’agaluka’, ‘ng’afumba’, ‘ng’atuemba’ ndiyo huwakilisha hali ya ukanushaji katika vitenzi vya Kisuba ilhali kiambishi ‘*si*’ na ‘*ha*’ katika kitenzi ‘*ninaruka*’, ‘*ninapika*’ na ‘*tunaimba*’ huwakilisha hali ya ukanushaji katika Kiswahili sanifu.

Aidha kwa mujibu wa Mgullu (1999) mizizi ya vitenzi inaweza kuwekewa viambishi vingi kuonyesha mambo mengi. Mfano huo unaweza kudhibitishwa katika Kisuba na Kiswahili vilevile.

	KUTENDA	KUTENDEA	KUTENDEKA
Kiswahili	Kupika	Pikia	Pikika
Kisuba	kufumba	Okufumbra	Ngeifumbra
Kiswahili	Kuimba	Kuimbia	Kuimbika
Kisuba	Okuemba	Okuembra	Ngeiemba
Kiswahili	Kuandika	Kuandikia	Kuandikika
Kisuba	Okujoja	Okujojra	Ngakuijora
Kiswahili	Kucheka	Kuchekea	Kuchekeka
Kisuba	Okuseka	Okusekera	Ngeiseka
Kiswahili	Kusoma	Kusomea	Kusomeka
Kisuba	Okusoma	Musomera	Ngeisoma

Kupitia kwa jedwali hili tunabaini kuwa viambishi vina uwezo wa kuathiri hali ya vitenzi katika lugha zote mbili. Kadhalika, Kisuba na Kiswahili huambisha vitenzi kutegemea nomino husika.

2.4.3 Mifano ya sentensi zinazosheheni viambishi

<i>Kisuba</i>	<i>Kiswahili</i>
Omugaka anywa owusara	Mzee anakunywa uji
Awagaka wanywa owusera	Wazee wanakunywa uji

Kupitia kwa jedwali hili, ni dhahiri kuwa mizizi ‘-anywa’ katika Kisuba na ‘nywa-’ katika Kiswahili huambishwa kulingana na idadi ya nomino husika.

Pamoja na hayo, upatanisho wa kisarufi pia imebainika katika Kisuba na Kiswahili sanifu. Mathaalan,

2.4.4 Sentensi za Kisuba na Kiswahili sanifu zinazosheheni upatanisho wa kisarufi

<i>Kisuba</i>	<i>Kiswahili</i>
K ino ne ekikapu ki ange	H iki ni kikapu cha ngu
W ino ne ewikapu wi ange	H ivi ni vikapu vy angu
R ino ne itoke wange	H ii ni ndizi yangu
G uno ne omuti wange	H uu ni mti wangu
R ino ne igi iria engoko	H ili ni yai la kuku
Ewifunguo ew ia nyumba iifu wi tekere	Funguo za nyumba yetu zi mepotea

2.4.5 Viambajengo vya sentensi

Kwa mujibu wa Habwe na Karanja (2004) viambajengo vya kimsingi vinavyounda sentensi ni maneno. Maneno huunda viambajengo vya viwango vya juu kama vile vikundi. Vikundi hivyo ni pamoja na kundi tenzi na kundi nomino. Aidha vishazi pia hujumuishwa katika kiwango hicho ijapokuwa ni vidogo kuliko sentensi. Kadhalika maneno tofauti hufanya kazi tofauti katika uundaji wa sentensi. Maneno hayo huainishwa katika makundi kulingana na maana na pia utendajikazi wao.

Aidha wanasarufi mapokeo waliweza kutambua aina mbalimbali za maneno walizoziita kategoria za maneno. Baadhi ya kategoria za maneno hayo ni kama nomino, vivumishi, vitenzi miongoni mwa kategoria nyingine.

2.4.6 Uchanganuzi wa viambajengo

Huu ni uchunguzi wa sentensi kwa mujibu wa ujirani wa viambajengo. Mathaalan, katika sentensi

KISWAHILI

KISUBA

Kichaka hiki kimefyekwa na mtu	Isaka rino ritembre no omuntu
--------------------------------	-------------------------------

Sentensi hizi zinaweza kuchanganuliwa kwa namna ifuatayo.

Neno `**Kichaka**` liko jirani na `**hiki**` kuliko lilivyo na `**kimefyekwa**` lhali neno `**kimefyekwa**` liko jirani na `**mtu**` kuliko lilivyo na `**hiki**`. Kwa hivyo, `**kichaka**` na `**hiki**` hujumuika kujenga kiima huku `**kimefyekwa**` `**na**` na `**mtu**` hujumuika kujenga kiarifa.

2.5 Kirai

Kirai ni tungo la kiisimu lenye zaidi ya neno moja lakini ambayo haina muundo wa kiima kiarifu. Kirai ni tungo ambalo halihusishi kitendo na yule anayekitekeleza. Aidha, ufafanuzi wa kimapokeo ni kuwa, kirai huonekana kama tungo kubwa kuliko neno lakini ndogo kuliko kishazi. Pamoja na hayo, kuna uwezekano wa kuunda kirai kutoka kwa kikundi kingine cha maneno. Kwa mfano kirai kielezi (RE) kinaweza kuundwa kutoka kwa kikundi tenzi (KT). Kadhalika, katika uchanganuzi wa sentensi, dhana ya kikundi hutumiwa kuashiria vile vikundi viwili vikuu yaani kikundi nomino na kikundi tenzi. Vikundi hivyo ndivyo huashiriwa kama kanuni muundo virai ambavyo vilibainishwa na Chomsky (1957). Kwa jumla, uchanganuzi wa kisintaksia haukamiliki

pasipo kurejelea msingi wa kanuni muundo virai. Kanuni hizi huwa na uwezo wa kuzalisha ruwaza za elementi za kiisimu.

Aidha, kwa kuwa dhima kuu ya utafiti huu ni ulinganisho wa sentensi za lugha za Kisuba na Kiswahili sanifu, inadhihirika kuwa sentensi za lugha hizi mbili hufuata ruwaza zifuatazo, mathaalan

Ruwaza ya kwanza

1		Kiima	Kiarufu	Yambwa tendwa
	Kisuba	Awaana	waria	ipapai
	Kiswahili	Watoto	wanakula	paipai

Ruwaza ya pili

2		Kiima	Kiarufu
	Kisuba	Ekikere we	kidumaduma
	Kiswahili	Chura	anarukaruka

Ruwaza ya tatu

3		Kiima	Kiarufu	Yambwa tendwa
	Kisuba	Awaala	wagonzizie	amavuta
	Kiswahili	Wasichana	wanapenda	mafuta

Ruwaza ya nne

4		Kiima	Kiarufu	Yambwa tendwa
	Kisuba	Katonda	amenyere	Kuegulu
	Kiswahili	Mungu	anaishi	mbinguni

Kutokana na majedwali haya, tunabaini kuwa, sentensi za Kisuba pamoja na Kiswahili husheheni kiima pamoja na kiarufu. Licha ya hayo, inabainika kuwa vikundi hivi huwa na vijenzi mbali mbali kwa mfano, kiima na kiarufu.

2.5.1 Kiima

Kwa mujibu wa Masebo na Nyangwine (2002) kiima ni sehemu ya sentensi ambayo hueleza yule anayetenda au anayehusika na kitendo fulani. Pamoja na hayo, mwandishi huyu anasema kuwa kiima ni sehemu inayokaliwa na jina au kikundi nomino na ambacho huwa ni kiambishi awali kipatanishi katika kitenzi kikuu. Kadhalika, kiima hutaja mada inayozungumziwa.

Kulingana na Obuchi na Mukhwana (2010) kiima huweza kuundwa kwa viambajengo vya kikategoria mathaalan,

Viambajengo vyaKiima katika Kisuba na Kiswahili sanifu

	Kiswahili	Kisuba
Viwakilishi nafsi	Mimi	Inze
	Wewe	Iwue
	Sisi	Ifue
	Yeye	Iyie
	Nyinyi	Inywe
	Wao	Iwo

Viwakilishi vionyeshi	Huyu	Ono
	Hawa	Wano
	Huu	Guno
	Hii	Gino
	Hili	Rino
	Haya	Gano
	Hiki	Kino
	Hivi	Wino
	Hii	Eno
	Hizi	Zino
Nomino na vivumishi	Mtoto mzuri	Omwana omulootu
	Ewirato ewilootu	Vyatu vizuri
	Iriino ilootu	Jino zuri
	Omwana omuwei	Mtoto mtundu
	Awaana wawei	Watoto watundu

Kupitia kwa jedwali hili, imebainika kuwa kiima huweza kuundwa na viambajengo vya kikategoria kama vile nomino, kiwakilishi au hata nomino pamoja na kivumishi.

2.5.2 Kiarifa

Kulingana na Obuchi na Mukhwana (2010) kiarifa ni sehemu ya sentensi ambayo aghalabu hufahamisha kuhusu kitendo kinachotekelezwa na nomino au kiima. Aidha kiarifa hutoa taarifa kuhusu kiima na pia hutaja jambo linalofanywa na kiima. Neno kuu katika kiarifu ni kitenzi. Kwa kawaida, kiarifu huja baada ya kiima na ni sehemu ya sentensi inayotoa taarifa kuhusu kilichofanywa au kitakachofanywa na kiima. Zaidi ya hayo, kuna uwezekano wa kiarifu kusimama pekee pasina kiima.

Vijenzi vya kiarifu

Katika lugha zote mbili, kiarifa husheheni sifa zifuatazo

- i. Kitenzi pamoja na nomino

Kisuba	Kiswahili
Afumre owuita	Amepika ugali

- ii. Kitenzi pamoja na kielezi

Kisuba	Kiswahili
Waingire munyumba	Wameingia nyumbani

- iii. Kitenzi, nomino na kielezi

	Kitenzi	Nomino	Kielezi
Kisuba	Ariire	owuita	munyumba
Kiswahili	Amekula	ugali	nyumbani

2.6 Uchanganuzi kategoria

Ili kuunda tungo katika lugha fulani kuna kanuni ambazo zinastahili kufuatwa ndiposa sentensi husika ziwe sahihi kisarufi. Kwa sababu hiyo, kanuni zinazotumika katika kuunda sentensi huwa ni kanuni za kisarufi ambazo huitwa kanuni zalishi. Kanuni hizi huzibainisha kanuni za kisarufi ambazo hurejelewa kama kanuni zalishi. Kadhalika, kanuni hizo huzibainisha kanuni za kategoria zinazotumika kutajia kategoria mbalimbali za viambajengo vya tungo kama vile kundi nomino (KN), nomino (N),

kikundi tenzi (KT), kitenzi (T), kitenzi kishirikishi, (Ts), kirai elezi, kirai kivumishi, na kirai husishi.

Katika sentensi za Kiswahili kwa mfano, uchanganuzi huu huweza kudhihirishwa .Mathaalan,

16.Juma anaenda shuleni

Sentensi hii inaweza kuandikiwa kanuni muundo virai kwa namna ifuatayo.

1. S → (KN KT)
2. KN → N
3. KT → T Kie (mahali)
4. N → Juma
5. T → anaenda
6. Kie → sokoni

Kanuni hizi humaanisha kuwa,

- i) Sentensi iandikwe upya kama Kundi nomino na Kundi Tenzi.
- ii) Kundi nomino liandikwe upya kama nomino (**N**)
- iii) Kundi Tenzi (**T**) liandikwe upya kama kitenzi (**T**) na Kielezi (**Kie**)

Kadhalika, sentensi za Kisuba vilevile huweza kuandikiwa kanuni miundo virai.Kwa mfano,

KISUBA**KISWAHILI**

Nyakiamo agiire musukuli	Nyakiamo ameenda shuleni
--------------------------	--------------------------

Sentensi hii inaweza kuandikwa upya kwa namna ifuatayo

1. S → (KN KT)
2. KN → N
3. KT → T Kie (mahali)
4. N → Nyakiamo
5. T → agiire
6. Kie → musukuli

Pamoja na hayo, kanuni hizi zinaashiria kwamba nafasi ya ishara zilizo upande wa kushoto huchukuliwa na zile ishara zilizo upande wa kulia.

Kadhalika, sentensi pia huweza kuchanganuliwa kwa kutumia dhana ya upanuzi uliyojikita katika mfanano wa ruwaza. Kigezo hicho hususan huweka mpaka kati ya jina la mtenda na tendo. Aidha upanuzi huhusu ubadilishaji wa muundo mmoja na mwingine uliofanana nao katika mazingira sawa.

Kwa mfano,

Kisuba		Kiswahili	
<i>Kiima</i>	<i>Kiarifu</i>	<i>Kiima</i>	<i>Kiarifu</i>
a)Omwaana	agwiire	Mtoto	ameanguka
b)Omwaana wange	agwiire uwiwi	Mtoto wangu	ameanguka vibaya
c)Omwana wange omulootu	agwiire uwiwi ukalu	Mtoto wangu mzuri	ameanguka vibaya sana.

Sentensi (b) na (c) zinachukuliwa kuwa ni upanuzi wa sentensi (a) Hali hiyo inadhihirika katika lugha zote mbili.

2.6.1 Elementi za Kirai Nomino

Kisuba

Kiswahili sanifu

Kirai nomino	Kirai kitenzi	Kirai nomino	Kirai tenzi
i. Omwana ono	agwire	Mtoto huyu	ameanguka
ii. Yeye	agwire	Yeye	ameanguka
iii. Nyakiamo	agwire	Nyakiamo	ameanguka
iv. Wamwifu omukalu	agwire	Kaka yangu mkubwa	ameanguka

Jedwali hili linaashiria kuwa nafasi ya kikundi nomino kinaweza kukaliwa na ,

viwakilishi - (mathaalan katika sentensi ya (ii))

nomino - (mfano huo upo katika sentensi ya (iii))

nomino pamoja na vivumishi (mfano huo unajitokeza katika sentensi ya (iv))

Zaidi ya hayo, kikundi tenzi vilevile husheheni sifa anuwai

2.6.2 Sifa za kundi Tenzi katika Kisuba na Kiswahili sanifu

	Kisuba		Kiswahili	
	Kikundi Nomino	Kikundi tenzi	Kikundi Nomino	Kikundi tenzi
i.	-	Agwiire.	-	Ameanguka
ii.	-	Eria emvwa.	-	Anakula samaki
iii.	-	Asomoka ni agia musukuli .	-	Anakimbia anapoenda shuleni

iv.	-	Aere omwaala okuria.	-	Alimpa msichana chakula
v	-	Emenyere mu omusiri.	-	Anaishi shambani
vi	-	Zisukre geza	-	Zimesukwa vizuri
vii	-	Aingire musukuli	-	Ameingia shuleni

Hapa tunabaini kuwa,

Sentensi ya 2.6.2 (i) ina kitenzi pekee

Sentensi ya 2.6.2 (ii) ina kitenzi, nomino

Sentensi ya 2.6.2 (iii) ina kitenzi, kishazi tegemezi na kielezi

Sentensi ya 2.6.2 (iv) ina kitenzi na kundi nomino.

2.7 Hitimisho

Sura hii imelinganisha sentensi za Kiswahili sanifu na za Kisuba, Vilevile, kazi hii imebaini tofauti zinazojitokeza baina ya lugha zote mbili. Kadhalika kupitia kwa sura hii, tunabaini kuwa tofauti zinazojitokeza katika Kisuba na Kiswahili ndizo labda zikawa visababishi vya makosa katika Kiswahili. Aidha mpangilio wa maneno katika lugha hizo mbili umeangaziwa, kwa hivyo ni dhahiri kuwa lugha zote mbili yaani Kisuba na Kiswahili zina sifa za upatanifu wa kisarufi. Vipatanifu hivi aghalabu hutumika katika vitenzi, vivumishi na viwakilishi. Zaidi ya hayo, viambajengo vinavyounda sentensi pia vimejadiliwa. Kwa hivyo kupitia kwa sura hii, tunabaini kuwa japo lugha huweza kufanana, vipo vipengele ambavyo pia huweza kuvitofautisha. Kwa jumla sura hii

imekuwa muhimu katika utafiti huu kwa kuwa tumeweza kubaini tofauti zinazojitokeza baina ya lugha hizo mbili na kwa hivyo tunakisia kuwa huenda tofauti hizo ndizo labda vikawa visababishi vya makosa katika Kiswahili. Kwa sababu hiyo sura ifuatayo imeangazia uchanganuzi wa makosa.

SURA YA TATU

UCHANGANUZI WA MAKOSA

3.0 Utangulizi

Katika sura hii tumeorodhesha makosa yanayofanywa na wanafunzi na kadhalika tumeelezea sababu kadhaa zinazosababisha makosa hayo. Ikumbukwe kuwa kila lugha huwa na miundo ya sentensi inayostahili kufuatwa na iwapo mtumizi lugha atahamisha maneno, msamiati au vipengele vya lugha yake ya kwanza na kuvitumia katika lugha ya pili, hivyo basi ataivuruga lugha ya pili.

Selinker (1972) anasema, makosa hutatiza mawasiliano. Aidha, mtaalam huyu amedokeza mikakati inayochochea kushuhudiwa kwa makosa katika tungo za wanafunzi.

Pia ameongezea kuwa, wanafunzi wengine huchukulia kuwa faridi za kiisimu na kanuni zinazotawala lugha yao ya kwanza ndizo pia hutawala lugha ya pili.

Kadhalika, Selinker (Ibid) ameongezea kuwa makosa katika kazi za wanafunzi huhusu vipashio vyote vya kiisimu kama vile,

- Fonolojia
- Mofolojia
- Sintaksia
- Semantiki

3.1 Makosa ya Kifonolojia

Kipashio hiki huhusu uchanganuzi wa mfumo wa sauti katika lugha fulani. Kila lugha huwa na mfumo fulani wa sauti mahususi ambao unastahili kufuatwa. Kwa hivyo, Kutozingatiwa kwa mfumo huo ndio husababisha makosa mengi katika tungo za wanafunzi. Mathaalan,

3.1.1 Udondoshaji au uchopekaji wa sauti

Udondoshaji ni utaratibu wa kukitoa kipashio fulani cha kiisimu katika silabi, neno, kirai au kishazi ilhali uchopekaji ni uingizaji wa irabu, kiyeyusho au konsonanti katika neno fulani.

Mifano ya makosa kutoka kwa data yetu yanayohusu udondoshaji na uchopekaji wa sauti ni kama ifuatayo.

17. ***Ana** badala ya hana

18. ***Akika** badala ya hakika

19. ***Hasubuhi** badala ya asubuhi

20. ***Aribu** badala ya haribu

21. ***Kusherekea** badala ya kusherehekea

3.1.2 Matumizi ya sauti /s/ badala ya sauti /sh/

22. ***Samba** badala ya shamba

23. ***Mastaka** badala ya mashtaka

24. ***Sida** badala ya shida

25. ***Sikamoo** badala ya shikamoo

26. ***Sirika** badala ya shirika

3.1.3 Uchopekaji wa irabu /u/

27. ***Mutume** badala ya mtume

28. ***Mukono** badala ya mkono

29. ***Musichana** badala ya msichana

30. ***Mukate** badala ya mkate

31. ***Muti** badala ya mti

Pamoja na hayo, wanafunzi hawa hukumbwa na tatizo la uhamishaji wa msamiati. Uhamisho ni utaratibu wa kisintaksia wa kukitoka katika sehemu fulani kiambajengo cha tungo na kukitumia katika lugha nyingine. Kwa mfano,

32. a)***Kuandikwa** kazi

- b) Otorwe kumirimo (Kisuba)
- c) Kuajiriwa kazi

33.a)***Kusikia njaa**

- b) Aurra omdenyo (Kisuba)
- c) Kuhisi njaa

34 a)*Gari ulipanda na wapi?

- b) Omtoka oninre ai (Kisuba)
- c) Uliabiri gari wapi?

35. a)***Waungaji** wa timu ya Gor Mahia

- b) Awaatu okuunga omukono etimu ya Gor Mahia (Kisuba)
- c) Mashabiki wa timu ya Gor Mahia

36. a)***Niliona** runinga

- b) Nyaona etivi (Kisuba)
- c) Kutazama runinga

37. a) *Nitasafiri **na** gari Kisumu

- b) Nyiza okugia no mtoka Kisumu (Kisuba)
- c) Nitasafiri kwa gari Kisumu

38. a) *Siwezi **kupima** mchezo huo na mwingine

- b) Ng'anyala kupima omuwayo guno nomuwayo gundi (Kisuba)
- c) Siwezi kulinganisha mchezo huo na mwingine

39. a) ***Anakunywa sigara**
b) Anywa esigara (Kisuba)
c) Kuvuta sigara

40. a) ***Kunywa chai na mandazi**
b) Nywa echae na mandasi (Kisuba)
c) Kunywa chai kwa mandazi

41. a) Enda na miguu

3.2 Makosa ya kimofolojia

- 42..*Mama amenipa vitabu **mbili** badala ya mama amenipa vitabu viwili

3.3 Makosa ya kisintaksia

43. a)*Mrefu mtoto amefika
b) Mtoto mrefu amefika
44. a)*Kipofu kilianguka kikaumia
b) Kipofu alianguka akaumia
45. a)*Mitume ilifika kwetu jana
b) Mtume alifika kwetu jana
46. a)*Shamba ya baba italimwa
b) Shamba la baba litalimwa

3.4 Makosa ya kisemantiki

- 47.*Kiatu cha mbwa kimefutwa kazi kwa sababu kumi ni kubwa kama hewa.

Sentensi hii haina maana kwa kuwa viambajengo vyake havihusiani ili kuleta maana kamili. Hivyo maneno huweza kuwa na maana yanaposimama pekee lakini yakakosa kuwa na maana katika tungo.

3.5 Uchanganuzi wa makosa ya kisintaksia

Kutokana na uchunguzi wetu, tumebaini kuwa makosa hujitokeza katika viwango vyote vya lugha. Kwa sababu hiyo, makosa hayafai kupuuzwa kwa kuwa makosa huathiri uandishi wa tungo. Aidha, wataalam wengi wameshughulikia swala hili la makosa na kuangazia visababishi vingi vya makosa. Aidha, kazi hii imechunguza makosa ya wanafunzi na vilevile kumulika chanzo cha makosa hayo kwa jumla. Kipengele kilichoshughulikiwa haswa ni kipengele cha sintaksia. Sintaksia ni taaluma ya sarufi inayochunguza jinsi vikundi vya maneno na sentensi mbalimbali hujengwa katika lugha. Pamoja na hayo, tawi hili huangazia kanuni za lugha husika. Kwa jumla, sehemu hii imechunguza sentensi hususan sentensi zisizokuwa sanifu. Kadhalika kazi hii pia imeainisha makosa katika insha za wanafunzi na kisha kubaini kila aina ya kosa na vilevile visababishi vya makosa hayo.

Kwa mujibu wa Lenon (1991) makosa ya kisintaksia huweza kutabiriwa. Makosa hayo ni kama yafuatayo.

Makosa yanayohusu vitenzi

- Makosa yanayohusu nomino.
- Makosa yanayohusu vivumishi.
- Makosa yanayohusu vipatanisho vya kisarufi.
- Makosa yanayohusu viambishi.

Ifuatayo ni makosa ya kisintaksia yanayojitokeza katika kazi za wanafunzi wa shule ya msingi ya Nyahera.

3.5.1 Makosa yanayohusu matumizi mabaya ya vivumishi vionyeshi

48 a)*Mti uliokatwa ni **ihuoo**

b)Mti uliokatwa ni **huu**

49.a)*Aliyetuzwa zawadi nyingi mno amefika **hukoo**

b)Aliyetuzwa zawadi nyingi mno amefika huko

50.a)*Kiti kilichovunjika ni **hichoo**

b)Kiti kilichovunjika ni hicho

51.a)*Kitabu **hichoo** kimechukuliwa na mwanafunzi

b)Kitabu hicho kimechukuliwa na mwanafunzi

Sababu za athari

Kutokana na utafiti huu, tumebaini kuwa kuna tofauti kati ya vivumishi vionyeshi vya Kisuba na vya Kiswahili sanifu. Tofauti hizo zinajitokeza kwa njia ifuatayo. Kiswahili sanifu kina vivumishi vionyeshi vya aina tatu yaani vivumishi vionyeshi vya karibu na mzungumzaji, vivumishi vionyeshi vya karibu na msikilizaji na hatimaye vivumishi vionyeshi visivyokuwa karibu na msikilizaji wala msemaji. Kwa upande mwingine, Kisuba kina vivumishi vionyeshi vya aina mbili pekee mathaalan, vivumishi vionyeshi vya karibu na msemaji na pia vivumishi vionyeshi vya karibu na msikilizaji wala lugha hii haina vivumishi vionyeshi visivyokuwa karibu na msemaji wala msikilizaji. Kwa hivyo, ukosefu wa kivumishi kionyeshi hicho ndicho huchangia katika kuwoko kwa makosa katika tungo za wanafunzi

3.5.2 Vivumishi vya sifa

Mifano ya makosa hayo ni kama ifuatayo

52. a)*Kiti **mzuri** imenunuliwa na baba
b)Kiti kizuri kimenunuliwa na baba
53. a)*Sungura **kizuri** litaliwa na fisi
b)Sungura mzuri ataliwa na fisi
54. a)*Yai **mzuri** litapelekwa sokoni
b) Yai zuri litapelekwa sokoni
55. a)*Dawa **mzuri** itamezwa na wagonjwa
b) Dawa nzuri itamezwa na wagonjwa
56. a)*Shamba **mzuri** litalimwa lote
b) Shamba zuri litalimwa lote
57. a)*Maji **mzuri** yameisha
b) Maji mazuri yameisha
58. a)*Meno **mzuri** hayatangolewa na daktari
b) Meno mazuri hayatangolewa na daktari

Sababu za athari

Kutokana na utafiti wetu tumegundua kuwa Kiswahili sanifu na Kisuba kina mfumo unaoshabihiana wa kuainisha vivumishi vya sifa. Aidha, katika lugha zote mbili, tumebaini kuwa, viambishi awali vya vivumishi hivi vinafanana na viambishi awali vya nomino inayovumishwa. Kwa hivyo, ni dhahiri kwamba, kisababishi kikuu cha matumizi mabaya ya vivumishi hivi ni athari ya lugha ya Kidholuo ambapo katika lugha hiyo,

mzizi **-zuri** haipachikwi kiambishi awali kulingana na nomino inayovumishwa. Vilevile, katika lugha hiyo, viambishi awali vya vivumishi vya sifa havifanani na viambishi awali vya nomino inayovumishwa.

3.5.3 Vivumishi viunganifu

Mifano ya makosa

59.a) *Shamba **za** baba limelimwa

b) Shamba la baba limelimwa

60.a) *Vyatu **za** shangazi vimechukuliwa na wezi

b) Vyatu vya shangazi vimechukuliwa na wezi

61.a) *Miti **za** kaka imekatwa

b) Miti ya kaka imekatwa

62.a) *Kiti **za** mjomba kimechukuliwa na wakora

b) Kiti cha mjomba kimechukuliwa na wakora

63.a) *Kuku **la** mama limetaga mayai

b) Kuku wa mama ametaga mayai

64. a) *Ngombe **za** baba zimechinjwa

b) Ng'ombe wa baba amechinjwa

Sababu za athari

Lugha za Kibantu husheheni vivumishi ambavyo huundwa kwa kiambishi tamati (-a). Kiambishi hiki huambishwa kwenye kiambishi ngeli kwa ajili ya kuleta upatanisho mwafaka.

Aidha, Kisuba na Kiswahili huambatanisha kiambishi tamati -a kutegemea ngeli husika. Hata hivyo, japo lugha zote mbili zina mfumo unaoshabihiana wa kuambisha kiunganifu hiki, wanafunzi hawa kutoka Suba wangali wanakumbwa na matumizi mabaya ya viunganifu hivi kwa sababu maneno mengi ya Kisuba ambayo yana maana sawa na ya Kiswahili hupatikana katika ngeli tofauti. Aidha makosa hayo yamesababishwa na uhamisho wa baadhi ya vipengele kutoka lugha ya kwanza hadi lugha ya pili.

3.5.4 Vivumishi vya pekee ‘o – te’

Mfano ya makosa

65.a) *Kichwa **zote** kitakatwa

b) Kichwa chote kitakatwa

66.a) *Shamba **yote** litalimwa

b) Shamba lote litalimwa

67. a) *Miti **yote** utakatwa

b) Miti yote itakatwa

68. a) *Viti **zote** zitapanguswa na wanafunzi

b) Viti vyote vitapanguswa na wanafunzi

69. a) *Ngombe **zote** zitaliwa na wakulima

b) Ng'ombe wote wataliwa na wakulima

Sababu za athari

Maneno mengi katika Kisuba ambayo yana maana sawa na ya Kiswahili yanapatikana katika ngeli tofauti. Kwa mfano, katika Kisuba nomino **shamba** na **kichwa** huainishwa katika ngeli moja. Vilevile nomino mbuzi na kiti pia huainishwa katika ngeli moja hali ambayo ni tofauti katika Kiswahili. Katika Kiswahili kwa mfano, nomino **mbuzi** hupatikana katika ngeli ya A-WA, ilhali **kiti** huainishwa katika ngeli ya KI-VI. Kutokana na hali hii tunabaini kuwa wazungumzaji wa Kisuba hukumbwa na tatizo la uhamishaji na pia uteuzi wa vipashio mwafaka wa kutumia katika sentensi.

3.5.5 Uhamisho wa msamiati

Mifano ya makosa

70. a) *Siwezi **kupima** mchezo huo na mwingine

b) Siwezi kulinganisha mchezo huo na mwingine

71. a) *Hamisi **alikunywa** sigara

b) Hamisi alivuta sigara

72. a) ***Waungaji** wa timu ya Gor Mahia walisafiri

b) Mashabiki wa timu ya Gor Mahia

73. a) *Nitaenda **na** gari Kisumu

b) Nitasafiri kwa gari Kisumu

74. a) *Juma **anasikia** njaa

b) Juma anahisi njaa

75. a) ***Kuandikwa** kazi

b) Kuajiriwa kazi

76. a) ***Kusikia** wivu

b) Kuona wivu

Sababu za athari

Wanafunzi huhamisha misamiati kutoka lugha yao ya kwanza na kuitumia katika lugha ya pili kwa sababu wanafunzi hawa hawana umilisi wa lugha ya pili. Aidha, wanafunzi hawa wanaposhindwa kupata msamiati mwafaka katika Kiswahili, wao huamua kutumia msamiati wa lugha ya kwanza ili kukidhi mahitaji yao katika matumizi ya lugha ya pili.

3.5.6 Upatanisho wa Kisarufi

Mifano ya makosa

77. a) *Punda **zilibeba** mizigo mizito

b) Punda amebeba mizigo mizito

78. a) *Kichwa **unauma** vibaya sana

b) Kichwa kinauma vibaya sana

79. a) *Ng'ombe **zimekula** nyasi

b) Ng'ombe amekula nyasi

80. a) *Viti **zimepotea** zote

b) Viti vimepotea vyote

81. a) *Miti **zimekatwa**

b) Miti imekatwa

82. a) *Samaki **zitaliwa** na wavuvi

b) Samaki wataliwa na wavuvi

83. a) *Mama amelima shamba **kikubwa** sana
b) Mama amelima shamba kubwa sana

84. a) *Kiwete **kilianguka** kikaumia vibaya
b) Kiwete alianguka akaumia vibaya

Sababu za athari

Lugha ya Kiswahili hupachika viambishi awali kwenye viwakilishi, vivumishi na wala sio nomino. Kwa hivyo lugha zote mbili huzingatia upatanisho wa kisarufi. Wanafunzi hawa kutoka Mfangano hukumbwa na matumizi mabaya ya vipatanisho hivi kwa sababu ya mambo kadhaa. Kama ilivyotajwa hapo awali, Kisuba huainisha nomino kama ‘**kichwa**’, na ‘**wanyama wengine**’ katika ngeli moja. Japo katika Kiswahili sanifu, wanyama wote huainishwa katika ngeli ya A-WA ilhali nomino ‘**kichwa**’ na ‘**kiti**’ huwekwa katika ngeli ya KI-VI. Kwa sababu hiyo, wanafunzi hawa wakati mwingine huchukulia kuwa faridi za lugha ya kwanza huweza kutumiwa katika lugha ya pili pasipo kusababisha makosa yoyote katika lugha hiyo.

3.6 Hitimisho

Sura hii imechanganua makosa anuwai katika tungo za wanafunzi. Kadhalika, makosa mengi yameorodheshwa na visababishi vyao kuangaziwa. Kutokana na sura hii, tunabaini kuwa makosa huwa na visababishi vingi. Pamoja na hayo, imebainika kuwa, makosa mengi katika lugha ya pili husababishwa na athari ya lugha ya kwanza.

SURA YA NNE

UCHANGANUZI WA DATA


4.0 Utangulizi

Katika sura hii, shughuli kuu ni kuchanganua data. Ni muhimu kutaja kuwa, makosa katika tungo za wanafunzi hujitokeza katika viwango vyote isimu, tofauti hujitokeza tu katika asilimia ya utokeaji.

4.1 Idadi ya makosa ya kisintaksia ikilinganishwa na makosa yasiyo ya kisintaksia

Vipashio vya lugha	Jumla ya wanafunzi walioandika tungo	Idadi ya makosa katika kila kipashio	Asilimia ya makosa
Fonolojia	16	13	81.25
Mofolojia	16	5	31.25
Sintaksia	16	8	50.00
Semantiki	16	1	6.25

Idadi ya makosa ya kisintaksia ikilinganishwa na makosa mengine





Baa grafu hii inaashiria kuwa, jumla ya wanafunzi walioandika insha walikuwa 16. Aidha, inabainika kuwa makosa yanajitokeza katika vipashio vyote vya Isimu ijapokuwa kwa asilimia tofauti. Mathaalan, makosa ya kifonolojia ndiyo yana asilimia ya juu ikilinganishwa na makosa mengine. Kadhalika, makosa ya kisemantiki ndiyo yenye asilimia ya chini zaidi.

4.2 Idadi ya makosa ya kisintaksia yanayosababishwa na athari ya lugha ya kwanza

Idadi ya makosa ya kisintaksia yanayosababishwa na athari ya lugha ya kwanza	Jumla ya wanafunzi	Asilimia ya alama
8	16	50
Idadi ya makosa ya kisintaksia yasiyosababishwa na athari ya lugha ya kwanza	Jumla ya wanafunzi	Asilimia ya alama
8	16	50

Idadi ya makosa ya kisintaksia yanayosababishwa na athari ya Kisuba



Kupitia kwa jedwali na baa grafu, tupata kuwa asilimia hamsini ya makosa ya Kisintaksia yanasababishwa athari za Kisuba kwa hivyo tunachukulia kuwa asilimia 50 ya makosa ya kisintaksia yaliyosalia yanasababishwa na visababishi vingine visivyo vya kisintaksia

4.3 Hitimisho

Katika sura hii tumetimia majedwali na baa grafu kuonyesha asilimia ya makosa katika kila kiwango cha lugha. Kadhalika, imedhihirika kuwa asilimia kubwa ya makosa ni ya kifonolojia ikifuatwa na makosa ya kisintaksia ilhali makosa ya kisemantiki ndiyo yana asilimia ya chini zaidi.

SURA YA TANO

MATOKEO NA MAPENDEKEZO

5.0 Utangulizi

Katika sura hii tumeangazia muhtasari wa yaliyomo katika utafiti huu. Vilevile tumetoa mahitimisho yetu kwa kurejelea malengo ya utafiti na mwishowe tumependekeza tafiti zaidi unaohitajika.

5.1 Muhtasari wa matokeo

Utafiti huu kwa jumla ulinuia kujibu maswali yafuatayo:

- Je, makosa yapi ya kisintaksia ambayo wanafunzi hufanya katika uandishi wa tungo?
- Je, ni makosa yapi husababishwa na tofauti za kisintaksia baina ya Kiswahili sanifu na Kisuba?
- Ni kiwango kipi cha makosa ambacho husababishwa na lugha ya kwanza.

Maswali haya yalijibiwa kwa ukamilifu kwa kuwa tuliweza kuorodhesha makosa ya kisintaksia na vilevile kiwango cha makosa yanayohusishwa na athari ya lugha ya kwanza. Aidha kupitia kwa kazi hii, tumebaini kiwango cha makosa ambacho nadharia ya uchanganuzi linganuzi huweza kutatua.

Aidha, utafiti huu pia ulinuia kutimiza malengo yafuatayo: Mathaalan,

kuainisha makosa ya kisintaksia katika kazi za wanafunzi kutoka kisiwani Mfangano.

Kadhalika, ilinuia kuhakiki makosa yanayojitokeza katika tungo za wanafunzi na hatimaye kubaini idadi ya makosa yanayoweza kuhusishwa na tofauti baina ya Kisuba na Kiswahili sanifu.

Kwa hivyo, kupitia kwa utafiti wetu, tumeweza kutimiza malengo hayo yote. Ni dhahiri kuwa makosa ya kisintaksia yameainishwa na mambo kadhaa kubainika. Tumetambua kuwa, makosa mengi ya kisintaksia katika kazi za wanafunzi hayasababishwi na athari ya lugha ya kwanza pekee bali makosa mengine husababishwa na athari nyingine. Aidha tulilinganisha sentensi za lugha mbili na kutambua kuwa, tofauti zinazojitokeza katika Kisuba na Kiswahili ndizo husababisha makosa katika lugha ya Kiswahili. Zaidi ya hayo, tuliweza kubaini asilimia ya makosa yanayosababishwa na athari ya lugha ya kwanza vilevile.

Licha ya hayo, kazi hii imebaini kuwa makosa mengi hujitokeza katika tungo za wanafunzi na pia ni wazi kuwa makosa hayo hujidhihirisha katika vipashio vyote vya lugha ijapokuwa kwa asilimia tofauti. Kadhalika, tumebaini kuwa asilimia hamsini ya makosa ya kisintaksia huhusishwa na athari ya lugha ya kwanza kwa hivyo, utafiti huu unachukulia kuwa, asilimia hamsini ya makosa yaliyosalia yanasababishwa na visababishi vingine.

Hatimaye, tumethibitisha kuwa baadhi ya haipotesia za utafiti huu zilikuwa za kweli kwa kuwa imebainika kuwa tofauti za kisintaksia baina ya Kisuba na Kiswahili huathiri matumizi ya Kiswahili miongoni mwa wazungumzaji wa Kisuba. Kadhalika kazi hii imeorodhesha na kuainisha makosa kadhaa yanayopatikana katika tungo za wanafunzi. Mbali na hayo, katika haipotesia yetu ya tatu, makadirio yetu hayakuwa ya kweli kwa kuwa sio asilimia arubaini ya makosa husababishwa na athari ya lugha ya kwanza kama

ilivyodokezwa bali tumebaini kuwa ni asilimia hamsini ya makosa husababishwa na athari ya lugha ya kwanza.

5.2 Mapendekezo

Ijapokuwa tumeshughulikia swala hili la athari ya Kisuba katika matumizi ya Kiswahili sanifu, tafiti nyingine inastahili kufanywa. Tungependekeza utafiti ufanywe zaidi, kubaini tofauti za kisintaksia baina ya sentensi ambatano na changamano za lugha hizo mbili. Pia ni matumani yetu kuwa walimu kutoka kisiwani Mfangano watakuwa na utaratibu mwafaka wanapoandaa na kufunza somo la Kiswahili.

Kadhalika tunapendekeza kuwa serikali ibuni sera itakayosaidia katika juhudi za ufufuaji wa lugha ya Kisuba kwa kuwa lugha hii imeorodheshwa na waandishi wengi kuwa imo miongoni mwa lugha zinazofifia.

5.3 Hitimisho

Imedhihirika kuwa kuna makosa mengi katika insha za wanafunzi. Makosa hayo hususan huhusu vipashio vyote vya kiisimu. Kadhalika ni wazi kuwa makosa katika tungo za wanafunzi yakichunguzwa kwa kina, mengi husababishwa na athari ya lugha ya kwanza. Pamoja na hayo, imedhihirika kuwa makosa hayo yanayofanywa na wanafunzi yanafaa kushughulikiwa kwa kuwa kila kosa lina kisababishi chake.

Marejeleo

- Bailey, N. Madden C. 7 Krashen (1974): *Is there a natural sequence in adult second language?* Vol. 23 No 2:235 – 243
- Bloom, P. (2002): *How Children learn meaning of words*, Cambridge: MIT Press
- Bloomfield, (1933): *Language*. New York: Hoilt Rinehart and Winston
- Bloomfield, (1933): *Language*. New York: Hoilt Rinehart and Winston dictionary 3rd edition: Dar es Salaam
- Brown, H.D. (2000): *Principles of language learning and teaching*. New York: Longman.
- Carol E Reed (1971): *The learning of language*, New York: Longman
- Carrol, J. B. (1964): *Language and thought*: Prentice – Hall, Englewood Cliffs
- Chomsky, N. (1957): *Syntactic structures*, The Hague: Mouton
- Corde, S. (1971): *Idiosyntactic Dialects and Error Analysis*, IRAL, Vol. 9:149-159
- Corder, S.P (1973): *Introducing applied linguistics*. Middlesex, Penguin.
- Corder S.P (1967): *Error analysis and inter-language*. Oxford: Oxford University Press
- David P.B Massamba (2004): *Kamusi ya Isimu na Falsaja*. Dar es Salaam: TUKI
- Ellis, R. (1984): *Classroom Second Language Development: A Study of classroom interaction and language acquisition*, Pergamon Press: Oxford
- Ellis, R. (1985): *Understanding Second Language Acquisition*. Oxford: OUP
- Ellis, R. (1986): *Understanding Second Language Acquisition*. Oxford: New York Oxford University Press
- Ellis, R. (1994): *The study of second language acquisition*. Oxford: Oxford University Press
- Ellis, R. (1997): *Second language acquisition*. Oxford: Oxford University Press
- Ervin – Tripp, S (1974): *Is second language learning like the first?* Tesol Quarterly, 8, 11-27
- Fisiak, (ed), (1981): *Constrastive Linguistics and the Language Teacher*: Oxford

- Gary Forlini et al (1990): *Grammar composition*. Englewood Cliffs: New Jersey
- Gass, S. M., and Selinker, L. (2001): *Second Language Acquisition: An Introductory Course* (2 Ed.). Mahwah, N. J. Lawrence Erlbaum Associates
- Guthrie, M. (1971): *Comparative Bantu*. Gregg, Farnborough
- Guthrie, Malcom (1948): *Classification of Bantu Language*, London: Oxford University Press for International African Institute
- Guthrie, M. C. (1948): *The Classification of Bantu Languages*. London: Oxford University Press
- Habwe, J. H. na P. Karanja (2004): *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*, Nairobi Phoenix Publishers.
- Halliday, M.A.K. (1975): *Learning how to mean*, London: Edward Arnold
- Jack C. Richards (1974): *Error Analysis Perspective on Second Language Acquisition*. Longman: London and New York
- Jarida la Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia (2004): *Kiunzi Huru Cha Kiswahili* (Haijchapishwa)
- Jefwa G. Mweri (2010): *Utangulizi wa Isimu*. Nairobi: Kenya Literature Bureau
- Kapinga M. C (1983): *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: TUKI.
- Lado, R. (1957): *Linguistics Across Cultures*. Ann Arbor: University of Michigan Press
- Larsen, Diane et al. (1992): *An Introduction to second language Acquisition Research*: London: Longman
- Larson – Freeman, D. & Long, M. H. (1991): *An Introduction to Second Language Acquisition Research*, Longman: New York
- Lennon, P. (1991): *Error and the very Advance Learner*, in IRAL (1991) Feb. Vol. 2911
- Lyons, J. (1968): *Introduction to theoretical linguistics*, Cambridge: Cambridge University Press
- Massamba, D.P.B. Kihoro na Hokoro J.I (1999): *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu*: TUKI Dar es Salaam
- Mbaabu, I (1992): *Sarufi ya Kiswahili*: Longman Kenya

- Mdee, J.S. (1986): *Kiswahili Maundo na Matumizi yake*: Dar Inter Continental Publishers LTD
- Mgullu, R. S. (1990): *The structure of Swahili Sentensi*, A Transformational Approach. M. A. Thesis, University of Nairobi (Haijachapishwa)
- Mgullu, R. S. (1999): *Mtalaa wa Isimu, Fonetiki, Fonolojia ya Kiswahili*. Nairobi: Longman Publishers Kenya Ltd.
- Nurse, D and G Philippon (2003): *Introduction in the Bantu languages* (D. Nurse and G. Philippon, eds.) Routledge: London & New York
- Omolo J. (2009): *From Olusuba to Dholuo, A case study of Language shift in Muhuru Division*: M.A Thesis.
- Otiende M.A (2013): *Athari za Kisuba katika matumizi ya Kiswahili sanifu kama lugha ya pili*: M. A. Thesis.
- Radford, A. (1981): *Transformational syntax*: Cambridge University Press
- Richard et al (1985): *Dictionary of applied Linguistics*, Longman: Harlow
- Richards, J. & Gloria P. Samson (1974): *The study of learner language* (J). In Richards, J.(ed.). (A)
- Richards, J. (1971): *Error Analysis and second language strategies* (J.) In *Language Science*, Vol. 17: 12-22
- Richards, J. (1974): *Error Analysis: Perspectives on second language acquisition* (A), Longman: London
- Rinehart and Winston Bloomfield, L. (1933): *Language*. New York: Hoilt Rinehart and Winston
- Samwel M. Obuchi na Ayub Mukhwana (2010): *Muundo wa Kiswahili Ngazi na vipengele* – Nairobi
- Swan, Michael (1980): *Practical English Usage*. Oxford; New York: Oxford University Press
- TUKI (1990): *Kamusi ya Isimu na Lugha*, Dar es Salam, Education Publishers and Distributors
- TUKI (2006) *English – Swahili Dictionary 3rd Edition*, Institute of Kiswahili Research of Dar es Salam

Waihiga, G. (1999) *Sarufi Fafanuzi ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn

Wyclife Bible Translators (2010): *Endagano Empia. The New Testament in the Suba Language of Kenya. Bible Translation and Literacy* (E.A) Kenya.

Yule, G. (1996): *The Study of Language*: Cambridge University Press

KIAMBATISHO